Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu

Asante, Ndugu Borders.

2 Mwaweza kuketi. Ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa, mkutanoni usiku wa leo, huku chini Port Alberni, miongoni mwa marafiki ambao ni wasafiri na wageni duniani, wanaokaa sasa hivi, wakingojea Kuja kwa Bwana, wapelekwe kwenye Mji ulio bora zaidi, Nchi bora zaidi ambamo hamna kifo, hamna huzuni. Nasi tunaungojea wakati huo wa Kuja kwa Bwana.

3 Si muda mrefu uliopita, nilipata fursa ya kuwa pamoja na mchungaji wenu, Ndugu Byskal. Nasi tulikuwa na ninii . . . safari ndogo pamoja baadaye, safari ndogo ya kuwinda huko kaskazini mwa British Columbia, naye akaniambia alikuwa anafanya umishenari kwa Wahindi, huku, huku—huku Kisiwani. Na, loo, siku zote nimetaka kumsaidia mtu ambaye anajaribu kuwasaidia Wahindi. Nimekuwa na matukio machache, huko Marekani, katika kuzungumza na Wahindi, Wanavajo, na Waapache, na wengi wao kule chini, na kuona imani ya ajabu sana. Naye Ndugu Eddie, ambaye hadhaminiwi na mtu yeyote, basi nikasema, "Labda wakati mmoja ningepata nafasi ya kuja kukusaidia, Ndugu Eddie."

Akasema, "Ningefurahia sana jambo hilo, Ndugu Branham."

4 Kwa hiyo tuko hapa usiku wa leo kwa mwaliko wake. Naye mwanangu, alikuja muda mfupi uliopita, naye husambaza kadi za maombi kuwaombea wagonjwa. Kwa kawaida hatufanyi hivyo kwenye usiku wa kwanza, wakati kutakuwa na mkutano mkubwa, mpaka tumetuliza kila mtu mpaka wafahamu. Lakini usiku wa leo, kwa kuwa tuna siku tatu tu usiku, nilisema, "Afadhali uzisambaze kadi za maombi, na—nasi tutawaombea wagonjwa usiku wa kwanza, ili tuweze kuanza moja kwa moja." Mimi . . .

5 Basi alikuja, akakutana nami, akasema, "Baba, kuna jambo moja tu baya kuhusu huu mkutano." Kasema, "Kuwa tu siku tatu usiku, inapaswa kuwa majuma matatu." Akasema, "Hawa ni watu wa kupendeza sana."

6 Sasa, hatuwahukumu watu kwa mali waliyo nayo, au jinsi wanavyoishi katika nyumba kubwa, jinsi wanavyovalia, tunawahukumu kwa yale yaliyo moyoni mwao. Hapo ndipo Mungu aishipo, moyoni. Basi unapoona urahisi, unyenyekevu,

kupendeza, na . . . hayo—hayo ndiyo tuyapendayo. Tunayapenda tu hayo. Nilizaliwa mara ya pili katika kundi dogo kama hili la watu, wakati mmoja, na mimi—mimi siku zote niliwazia walikuwa—walikuwa watu walio wanyenyekevu sana, wazuri zaidi, na hao ndio nimeishi nao duniani, nami ninaamini nitaishi pamoja nao Utukufuni katika nyakati zisizo na kikomo zijazo.

7 Nami ninakumbuka tukio langu la kwanza la kuwahudumia Wahindi, nami nadhani hawa walioketi hapa mbele ni Wahindi, nafikiri tu hivyo. Nami nina furaha sana kuwa pamoja nanyi. Jamani, Wamarekani halisi, hiyo ni kweli, Mmarekani halisi, wale ambao Mungu aliwapa Marekani, Wahindi. Kwa hiyo ninashukuru sana. Wao ni . . .

8 Chini kabisa ndani ya mishipa yangu mnatiririka damu kidogo. Bibi ya mama yangu anatoka kwenye hifadhi. Na daima nimehesabu hilo kwamba ni mojawapo ya majaliwa makuu sana, kusema ya kwamba ndani yangu kuna sehemu, Mmarekani kweli. Kwa maana kuna msingi kidogo, mahali fulani, wa damu ya Kihindi ambayo ninaifurahia sana, nashukuru sana. Na sikuzote nimetaka kuwahudumia, kwa sababu mama yangu alikuwa mama halisi. Alienda tu nyumbani Utukufuni hivi majuzi, mwanamke mkongwe, akiwa na tukio halisi la kuwa salama mikononi mwa Kristo. Nilimshika mikono wakati Mungu alipokuja na kumchukua, hivi majuzi tu. Nami najua alivyokuwa, na jinsi alivyokuwa mpenzi wangu wa moyoni, na mama, nami na—nampenda. Nami nina furaha sana usiku wa leo kuwahudumia hawa watu.

9 Nilikuwa Arizona ninii . . . moja . . . mwanzoni mwa huduma yangu, na kulikuwa . . . Usiku mmoja, wakipitia kwenye mstari wa maombi, walikuwa . . . Nilikuwa nikiwahudumia watu wanaozungumza Kihispania, na kulikuwa na Wahindi wawili, wawili wa kwanza niliowahi kuwahudumia. Basi mmoja wao alikuwa mlevi sugu, na huyo mwingine alikuwa na kifua kikuu, alikuwa kwenye machela, ugonjwa.

10 Ndipo nilipowaona wakiingia mstarini, nilisimama kwa muda kidogo, kisha nikasema, “Ngojeni kidogo.” Nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, hii ndiyo mara yangu ya kwanza, sasa, ku—kuwaombea, wale ninaowaita, Wamarekani ukoo safi.” Nikasema, “Kama—kama ukitaka niwahudumie na kwenda kwenye kabila lao, kama utawaponya, ninakuahidi nitaenda.” Ndipo nikawaombea, na kabla sijafika kwenye mkutano mwingine huko California, yule mlevi sugu alikuwa amepoteza upendo wote wa pombe na akawa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, naye yule mwenye kifua kikuu alikuwa, katika muda wa juma moja, alitangazwa na da—daktari, huko kwenye hifadhi, ya kwamba amepata nafuu na ni mzima. Kwa hivyo nikarudi kwenye—kwenye kabila la Apache. Sitasahau hilo kamwe.

11 Natumai sitachukua muda mwingi mno sasa. Daima nimezoea kuzungumza kwa muda mrefu mno. Kila mtu sikuzote huniambia mimi huzungumza kwa muda mrefu sana; hiyo ni kwa wazungu, si kwa Wahindi. Naam, bwana. Sisi . . . Nilihubiri mahubiri mafupi hivi majuzi kwenye maskani yangu nyumbani, saa sita tu, hizo tu ndizo nilizohubiri. Kwa hiyo . . . Lakini sisi—sisi Wahindi hatuna haraka, mnajua. Kwa hiyo tu—tuna muda mwingi wa kusikiliza.

12 Na hivyo wakati . . . Kwa hiyo, hii . . . usiku huo walinipeleka kwenye hifadhi. Na loo jamani, sijawahi kuona wengi namna hiyo! Wao . . . Ilikuwa picha nzuri. Walikuja kwa mabehewa yao, na kila mahali, imetangazwa kote kwenye hifadhi, nao wakaketi chini ardhini. Nilikuwa nimesimama kwenye kipandio kidogo cha barazani, kanisa dogo, yapata kama hili. Kulikuwa na Wahindi wengi ndani, na . . . Lakini loo, jamani, ninii . . . wote, nusu ya hilo kabila, ama zaidi, walikuwa wameketi huko nje. Loo, ninakadiria, elfu nne ama tano, kitu kama hicho, wamekusanyika nje.

13 Na kwa hiyo, nilikuwa nikizungumza kutoka kwenye vipandio vya kanisa, kanisa dogo la Assembly of God. Naye huyu mmishenari alikuwa amehudumu huko kwa muda fulani. Na kwa hiyo, nilikuwa na mkalimani mmoja, wasingeweza kuelewa Kiingereza. Na kwa hiyo, nilikuwa na mkalimani mmoja, ambaye alikuwa ni mama.

14 Vema, nilijaribu kwa njia rahisi niliyoweza kuwawekea Biblia, na—nami nakumbuka waliketi tu na kutazama, mwajua. Ninasema hivi kwa upendo, Mhindi, wakati anaposhawishika, habanduki kamwe. Lakini yeye ni kitu kama kumlisha farasi, yeye hali kwenye zizi lingine. Mnaona? Anangoja mpaka awe na uhakika wa kile anachozungumzia, kwa hiyo walikuwa wakingoja. Na kwa hivyo alikuwa akiangalia aone kile nitakachosema.

15 Nami nikaendelea kuwaambia, nikasema, "Sasa, mimi ni kura moja tu, mtu mmoja hapa, nchini." Nikasema, "Ninaamini kwamba kulikuwa na namna fulani ya njama ambayo haikupaswa kufanyiwa Mhindi." Nikasema, "Ni—ni—ninaamini kwamba, kama taifa lingine lingetuvamia na . . . kungekuwa na hisia mbaya kwetu." Lakini nikasema, "Mimi . . . Hivyo—hivyo ndivyo afanyavyo mwanadamu." Nikasema, "Nitawaambia, kuna Mtu awapendaye, huyo ni Yesu Kristo, Naye atakuwa papo hapo pamoja nanyi mpaka mwisho wa safari."

16 Wakaketi . . . Sasa, kidogo walikuwa wa kipekee. Niliomba mstari wa maombi. Vema, katika siku hizo tulipoanza kwa mara ya kwanza, mbona, hatukusambaza kadi za maombi, hiyo ndiyo njia pekee ya kuweka utaratibu, na kwa hiyo, sikuwa na kadi za maombi, nami nikasema, "Je, kuna mtu yeyote, huko nje, anayetaka kuombewa?" Mkalimani akasema vivyo hivyo,

hakuna mtu aliyesogea. Vema, nikawazia, "Jamani, nadhani sitakuwa na mstari wa maombi."

17 Kwa hivyo katika dakika chache, huyo mmishenari wa Kihindi akarudi, pamoja na mmishenari mzungu, na kuwachukua baadhi ya watu kutoka humo ndani. Wa kwanza kutoka nje alikuwa mwanamke mkubwa, mwenye nguvu. Mara tu yeye. . .Nikamtazama usoni. Wengi wenu, nadhani Ndugu Eddie amewaambia kuhusu huduma hii. Alikuwa na ugonjwa wa kijamii, si kwa sababu hakuwa mwadilifu, bali kwa sababu ya jinsi alivyolazimika kuishi. Ndipo nilipomwambia jambo hilo, alinitazama kiajabu sana. Kwani nilijuaje hilo? nikiisha kulielezea katika Maandiko.

18 Aliyefuata alikuwa mvulana mdogo mwenye makengeza. Si—sitasahau hilo kamwe. Naye mama . . . Nikasema, "Unaamini kwa ajili ya mvulana huyu?" Naye mwa—mwanamke huyo akadhani nilimwuliza shida ya huyo mvulana, kwa hivyo akamshika tu kwa nywele na kumrudisha nyuma, macho yake madogo yalikuwa na makengeza. Kwa hiyo nikamnyanyua huyo jamaa mdogo, na kumpa kipande cha chingamu, unaona, hakufahamu Kiingereza, kitu kingine cha kumfanya atulie, nione ni njia gani Roho Mtakatifu alikuwa akitenda kazi. Basi nikamtuliza na kumlaza begani mwangu.

19 Nami nikasema, "Baba wa Mbinguni, kama ninaweza kupata neema machoni Pako, na iwe sasa." Unaona? Nikasema, "Ninaomba uyanyooshe macho ya huyu mvulana mdogo, ili kwamba watu waone kuna. . .Hawaelewi hili, nao hawana budi kuelewa kwamba Unawapenda." Basi mara niliposema hivyo, nikaangalia nje, kulikuwa na ono, huyo mvulana mdogo angeweza kuona.

20 Nikasema, "Sasa, kabla sijamtoa mabegani mwangu, kama macho ya mvulana huyu mdogo siyo sawa, kama kawaida," nikasema, "basi mimi—mimi ni nabii wa uongo. Lakini ikiwa yako sawa, je, mtamwamini Mungu?"

Ndipo basi mkalimani akasema, "Naam."

Sikuangalia kamwe, niligeuka tu namna *hiyo*, nao wakaanza kupiga mayowe. Huyo hapo, angeweza. . .macho yake yakiwa yamenyooka kabisa.

21 Kwa hiyo basi, aliyefuata, basi aliyefuata alikuwa ni msichana mdogo, naye alikuwa wa mmoja wa hao, nafikiri, mmoja wa hao viongozi katika hilo kabila, naye alikuwa kiziwi na bubu. Na kwa hiyo, nikawafanya wamfanye aniangalie kidogo tu. Nikasema, "Naam, yeye ni kiziwi na bubu pia, na kilichosababisha hayo kilikuwa ni homa aliyokuwa nayo yapata miaka minne iliyopita, na kumwacha akiwa kiziwi na bubu."

Mkalimani akauliza kama. . .akasema hivyo. Naye huyo mama akatikisa kichwa, yule mama aliyekuwa naye, yule dada wa Kihindi, "Hiyo ilikuwa kweli."

22 Nami nikasema, "Sasa, siwezi kuyafungua masikio yake, mimi—mimi ni mtumishi tu, siwezi. Lakini iwapo—iwapo nitamwombea, unaamini Mungu atamponya?" Aliamini. Kwa hiyo nikamshika msichana huyo mdogo mikononi mwangu, nami nikamwombea, kisha nikamweka chini. Ndipo nikamwambia mkalimani, nikasema, "Sasa, sema tu kwa Kihindi, lugha yao, lu—lugha ya Kiapache, kile ninachosema kwa Kiingereza."

"Sawa."

Nami nikasema, "Je, unampenda Bwana Yesu?"

23 Naye akasema. Akamwangalia kigeni sana, angeweza kusikia. Nami nikasema, "Mwambie aseme nilichosema." Basi niliposema hivyo, aligeuka, akanitazama, aliweza kusikia. Mnaona? Ndipo aliporudi namna *hii*, nilifanya [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] akageuka, akatazama, aone ilikuwa ni wapi. Nikasema, "Sasa mwambie aseme, 'Nampenda Yesu.'" Naye akamunyamunya kitu fulani. Sikuwa nimeisikia hiyo lugha kamwe.

Nikasema, "Unajua, atazungumza vizuri baada ya muda mfupi."

24 Naye huyo mama, aliyekuwa anatafsiri, akageuka, akasema, "Yeye ongea vizuri sana sasa." Alikuwa akiongea kwa lugha yake mwenyewe. "Anaongea vizuri sana sasa."

25 Sasa, nena kuhusu mstari wa maombi! Mabawabu mia mbili wasingeweza kuwashikilia, hivyo tu. Kulikuwa na mstari wa maombi, sijapata kuona kama huo, kama tu mkanyagano. Na kila mtu alitaka kuingia kwenye huo mstari wa maombi, wala hatungeweza kuwazuia.

26 Basi kulikuwa na . . . Aliyefuata alikuwa ni mwanamke mkongwe. Sasa, wao ni fukara sana, lakini wao ni watu wa Mungu. Naye alikuwa mkongwe sana, naye alipaswa kuwa wa pili mstarini, kuja *hivi*, ila tu jamaa mdogo, jasiri mdogo yapata urefu *huu*, ameumbika imara, mwenye nguvu sana, alipenya tu, na kumpita kila mtu, naye ndiye angefuata. Vema, hatungeweza kumfanya aelewe.

27 Kwa hiyo Ndugu Moore, mtu aliyekuwa pamoja nami, alichukua tu . . . ilimbidi kumshika mikono, na kujaribu kumwambia kwamba haikuwa sawa kwake kufanya hivyo, mama huyu ndiye aliyefuata. Hatimaye wakamfanya aelewe. Basi maskini huyo mama mkongwe, wakamtoa chumbani, maana hawa walikuwa wameanza kwanza, wakawaacha waje kwanza.

28 Vema, huyu hapa anakuja, nami nikamwona. Sasa, i—inasikitisha jinsi yeye . . . Alikuwa na vijiti viwili vya ufagio, vilivyokatwa, na tundu limetobolewa kupitia kipande kidogo cha mbili kwa nne ili kufanya sehemu ya msalaba ya hilo gongo, huku limefungwa kwa matambara. Basi alipotoka nje,

angeweza tu kuweka magongo hayo namna *hii*, basi . . . Yabisi kavu. Mnaona? Asingeweza kusogeza miguu yake namna *hiyo*. Ndipo akaweka nje magongo haya, naye . . .

29 Nilisimama tu kimya, nikaacha aje. Naye akanikaribia moja kwa moja, kisha akaangalia juu. Maskini bi-kizee huyo alikuwa akitetemeka kwa ugonjwa wa kupooza, makunyanzi manene, makubwa mno, mashavuni mwake. Alipoangalia juu, nywele zake zenye mvi, zilizofunikwa kwa ngozi, zikining'inia mgongoni mwake, machozi yalikuwa yakitiririka chini, kupitia makunyanzi hayo. Nikawazia, "Mama wa mtu fulani." Akasimama hapo.

30 Ndipo aliponitazama *hivyo*, sikumwambia lolote. Kidogo akatabasamu tu, akanyoosha mkono na kuchukua moja ya magongo hayo, akaliweka pamoja na gongo hilo lingine, akanikabidhi, kisha akaondoka pale akitembea vizuri tu kama mtu yeyote. Mnaona? Mnaona? Nini? Mnaona? Nikasema, "Vipi . . . ?" Nikamwuliza ilikuwaje akawa na imani hiyo.

Akasema, "Kama Yeye nyosha macho yenye makengeza, Yeye nyosha miguu." Hiyo ilikuwa nzuri vya kutosha kwake. Mnaona?

31 Imani rahisi tu, hiyo ndiyo tu inayohitajika. Unapojaribu kulitafakari, huwezi kumwelewa Mungu, huna budi kumwamini Mungu. Unaona? Huna—huna . . . Haihitaji elimu, hiyo hutupeleka mbali na Mungu, kadiri tunavyojua mengi katika elimu, ndivyo tunavyozidi kwenda mbali na Mungu. Hicho ndicho kikwazo kikubwa kuliko vyote Injili imekuwa nacho, ni kuelimisha. Kisha wanaanza kuwazia kwamba wanajua mengi kuliko Mungu. Lakini ukijifanya rahisi, na kumwamini tu, hilo tu ndilo lote linalohitajika.

32 Kitu kingine kidogo kabla ya kumalizia ushuhuda wangu. Niliomba usiku kucha. Ilikuwa inaelekea yapata saa tisa au kumi alfajiri, nisingeweza kusimama tena, na ilinibidi kusimamisha upambanuzi baada ya saa kumi na moja au kumi na mbili, nilikuwa tu nikiwawekea mikono. Ndipo nikaanza kuona wakivuka . . .

33 Sasa, m—mto unapitia moja kwa moja kwenye hifadhi, na huo ni Salt River, unaopitia kwenye hifadhi, nao unakuwa na kina kirefu mahali mahali. Ndipo nikaona Wahindi waliokuwa wakiingia walikuwa wamelowa maji kote kiunoni mwao. Kwa hiyo nikasema, "Kwani kuna nini?" kwa mkalimani.

34 Naye akasema, "Kwanza kabisa walidhani wewe ni mwongo," kasema, "lakini wanajua ni ukweli sasa, nao wanawabeba wapendwa wao. Kivuko hicho kiko kama maili kumi na tano hapa chini, lakini wanatembea moja kwa moja kuvuka kuja *huku* pamoja na wapendwa wao, wakiwabeba usiku kucha," wapate tu kuwa huko usiku mmoja.

35 Aliyefuata mstarini, akiingia, akitembea jukwaani, alikuwa ni mzee. Walikuwa wametengeneza machela ya kumbebea,

walichukua ubao mpana *hivi*, nao walikuwa wameweka fimbo kuukingama *hivi*, na fimbo *huku*. Ndipo wakamchukua huyo mzee na kumlaza pale juu, nao mguu mmoja umening'inia mwishoni mwa fimbo, na kisha mikono yake namna *hiyo*. Kulikuwa na vijana wawili wakubwa, wenye sura nzuri, waliombeba, wamesimama tu pale, nayo midomo yao ni bluu, ikitetemeka. Kuna baridi jangwani, kunakuwa na baridi kali asubuhi namna hiyo. Walikuwa wakitetemeka, wakingoja, niliwaona wakija mstarini.

36 Niliendelea kuwaombea hao watu, nikiwawekea tu mikono, nikiomba wakati wakipita. Kwa hiyo jamaa huyu akasimama pale, alikuwa akitetemeka, akiwa amemshika namna *hiyo,* yule mzee. Nikasema, "Umelowa maji." Kasema . . . Akanitazama, nikasema. "Unazungumza Kiingereza?"

Kasema, "Kidogo."

Nikasema, "Hivi huogopi, utashikwa na nimonia?"

"Hapana." Kasema, "Yesu Kristo ananitunza tu. Nilileta baba yangu."

"Hmm, hmm." Nikasema, "Ni nani huyo upande mwingine?"

"Ndugu yangu."

37 Nikasema, "Mlete." Asingeweza kuzungumza Kiingereza. Jamaa huyo alikuwa amepooza, akitetemeka namna *hii*, ambao ulionekana kuwa ni ugonjwa mbaya miongoni mwao, huo na glakoma. Kwa hiyo ni—nikasema, "Bwana, unamwamini Bwana Yesu Kristo?" Naye mwanawe akamwambia hivyo, mwajua, naye akatikisa kichwa chake kwamba anamwamini. Nikasema, "Sawa. Kama unaamini sasa, imani rahisi tu, Mungu atakuponya."

38 Nikaweka mikono yangu juu yake, nikasema, "Baba wa Mbinguni, baba yao, bila shaka alihangaika siku nyingi kuwapa chakula hao wavulana." Nikasema, "Sasa, wao—wao wanaamini, nao walimbeba wakamvusha mto ule pale, na—na kutoka mbali sana huko kwenye hifadhi, pengine imechukua saa nyingi kumfikisha hapa." Nikasema, "Hakika, ninaamini ya kwamba Wewe utamponya. Katika Jina la Bwana Yesu, ninaomba; ninaweka maombi yangu juu ya madhabahu Yako na kuamini." Nami nikasema, "Vema. Sasa, mpeleke nyumbani, wala usitie shaka."

"Asante," wakaanza kuondoka.

39 Nami nikasema, "Mwingine." Wakamleta mwingine, baada ya muda kidogo nikasikia mtu fulani (nilikuwa kwenye hii baraza) akipiga kelele, na Wahindi wote wakipiga kelele na kupiga mayowe. Nikatazama kule chini, naye yule mzee alikuwa amebeba ule ubao mabegani mwake, akitoka, akimpungia kila mtu mkono. Hiyo ilifanya . . . Hiyo . . . Sasa, mnaweza kuona

ni kwa nini ninapenda kuwahudumia Wahindi. Mnaona? Wanaamini.

40 Sasa, nataka . . . Niko hapa kusema hivi, ndu—ndugu yangu, dada, na kwa wazungu pia, mnaona, kwenu nyote. Tuko hapa nchini, na hali ya hewa, na kadhalika, ikibadilisha rangi zetu za ngozi. Mungu, kwa damu moja, aliwaumba watu wote, sote tulitoka kwa Adamu, tuwe weupe, wa kahawia, weusi, manjano, wekundu. Vyovyote vile tulivyo, sisi sote tumetoka katika mti mmoja, Adamu, mtu wa kwanza wa Mungu, na kwa hiyo, sisi ni kama wasafiri.

41 Kila mahali, nimezunguka ulimwengu mara kadhaa, wala bado sijapata kuona, ambapo tuliwahi kupata watu waliompenda Mungu, ila kwamba walikuwa ni watu wazuri sana. Nimekuwa huko chini ambapo hawakujua hata mkono wa kulia na wa kushoto ni upi. Hawakujua hata kuvaa nguo, walikuwa uchi wa mnyama, hawakujua lolote, hata hawakujua walikuwa uchi, wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, kamwe hawajui lolote kuhusu hilo. Lakini ukisimama hapo, na kuwaacha wampokee Kristo, na kumpokea Roho Mtakatifu wakisimama hapo, wanafanya mambo yale yale mnayofanya. Mnaona? Na bila kuambiwa, wanafanya hivyo hata hivyo, mnaona, hiyo inaonyesha ya kwamba Roho Mtakatifu ni wa ulimwengu wote. Mnaona? Yuko kila mahali, ni yeye yule, kote ulimwenguni.

42 Kwa hiyo hapo wakati huo mkuu utakapokuja, wakati Yesu wetu atakapowasili, kutakuwa mmoja katika . . . wawili katika kitanda kimoja, ambako ni wakati wa usiku, "Nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja," wawili kondeni, ambako ni mchana, upande mwingine wa dunia, "Nitamtwaa mmoja, na kumwacha mmoja." Mnaona, itakuwa ni kila mahali. Ufufuo, Unyakuo mkuu wa Kanisa utakuja, nasi sote tutaenda Nyumbani pamoja. Ndipo wazee watageuka kuwa wachanga, na, loo, utakuwa wakati mzuri sana.

43 Sasa, marafiki Wakristo, na kwa Ndugu Eddie, na wafanyakazi wa ndugu wahudumu hapa, na kwenu mlio huko nje, hatuko hapa kuwakilisha kanisa lolote la kimadhehebu. Tuko hapa kwa niaba ya upendo wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Tuko hapa, sio kufanya washiriki wa kanisa fulani, bali wa *lile* Kanisa. Na kuna Kanisa moja tu hata hivyo, na hilo ni Kanisa la Bwana wetu Yesu Kristo. Na hatujiungi Nalo, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," ambao ni Kanisa la Kristo, Bibi-arusi Wake, hivyo ndivyo tunavyokuwa Wakristo. Nasi tunampenda, nami najua kila . . . hao wengine wanampenda.

44 Sasa, kweli tuna mashirika, madhehebu, hayo ni sawa. Hiyo ni sawa, lakini mradi tu hawatachora mstari, waseme, "Sisi Ndio, na nyinyi sio." Unaona? Ni . . . Sisi ni—sisi sote ni

Hilo, kama tumebatizwa katika huo Mwili. Nami nimesema, "Nimekuwa na familia ya Branham sasa kwa zaidi ya miaka hamsini, na kamwe hawakuniomba nijiunge na hiyo familia." Mnajua ni kwa nini? Nilizaliwa ndani yake, ni—nilikuwa Branham kwa kuzaliwa. Na hivyo ndivyo tunavyokuwa Mkristo, ni kwa kuzaliwa. Haijalishi sisi ni wa kanisa gani, sisi ni Wakristo kwa kuzaliwa. Halafu kwa kuzaliwa, kunaleta Uhai Wake ndani yetu nasi tunatoa Uhai Wake kupitia kwetu. Mnaona?

45 Wewe. . . Kama ungeweza kuchukua utomvu, uhai, kutoka kwenye mti wa tofaa na kuuweka kwenye mzabibu, mzabibu huo ungezaa matofaa, mnaona, kwa sababu uhai uliokuwa. . . huzaa matofaa, hiyo chembe iko kwenye huo uhai, nao ungezaa tofaa kwenye mzabibu. Inategemea ni uhai wa aina gani ulio ndani yake. Mnaona? Hiyo ni kweli.

46 Sasa, kama ungeweza kuchukua mpichi na mpea, na kutoa u—uhai kwenye huo mpichi, uutoe tu uhai wote, na kuuweka kwenye mpea, kila sehemu ya uhai, hamna uhai wa mpea tena ndani yake, bali uhai wa mpichi, ungezaa majani ya mpichi. Na ungekuwa—ungekuwa na majani ya mpichi, na kuzaa mapichi, kwa sababu una uhai wa mpichi ndani yake.

47 Na haijalishi mwenye dhambi ni mbaya kiasi gani, ni mwovu kiasi gani, ni wabaya kiasi gani, ni asiyeamini kiasi gani, kama unaweza tu kuondoa uhai huo wote wa kale wa kutokuamini, unaona, uuweke Uhai wa Kristo ndani yake, atakuwa mtu tofauti. Hiyo ni kweli. Ha—hakika atakuwa, hakika atakuwa mtu tofauti.

48 Nami ninaamini Biblia kuwa ni Neno la Mungu. Mnaona? Ninaamini kuwa ni kamilifu. Nayo. . . wala hakuwezi kuondolewa chochote, wala kuongezewa chochote Kwake.

49 Sasa, kimsingi, asili yangu mimi ni Mwairishi, kwa hiyo basi, watu wangu walikuwa Wakatoliki. Lakini katika kanisa le-,. . . nyumbani kwangu hawakuwahi kufunga ndoa kanisani, mpaka. . . hawakuwa wafuasi wa chochote, na huko ndiko nilikopata wito wangu. Pengine mnavyo vitabu hivyo, na mmevisoma, vya *Hadithi Ya Maisha Yangu.* Ndipo nikaitwa kwenye huduma hii.

50 Sasa, nilipoanza kuwa Mkristo, ama kumwamini Kristo. . . Tangu mvulana mdogo ilianza na mimi, nilipokuwa, kwanza, nilipozaliwa. Nilipozaliwa, Nuru hiyo, mnayoiona kwenye picha hapa, ilikuwa inaning'inia juu ya kitanda kidogo nilimozaliwa, huko juu sana milimani, bila hata sa—sakafu ya mbao, udongo tu. Wala hatukuwa hata na. . . hata hawakuwa na meza, Baba alikata kipande cha kisiki, na kukiwekea miguu kiwe meza. Nami nilikuwa na kitanda kidogo kilichotandikwa makapi ya mahindi. Sijui kama mnajua kile. . . makapi ya nafaka, kapi, nao wakatengeneza mto na kitanda kutoka kwa hayo. Na hapo ndipo

nilipozaliwa, saa kumi na moja asubuhi moja. Wala hatukuwa hata na kioo dirishani, mlango mdogo tu unaousukuma nje, na—na ndipo Nuru hiyo ikaingia; ndipo inaonyesha ya kwamba Mungu si lazima awe na jumba la kifalme la kujia, nyumba nyenyekevu tu, mtu yeyote atakayeamini.

51 Na sasa, ninaamini Neno la Mungu ni kamilifu sana hata hatuwezi kulifasiri vibaya. Ni lazima tu tulifundishe jinsi lilivyo, na kuliishi jinsi linavyofundishwa. Sasa, na—naamini sasa . . . Sasa, kama vile kasisi alivyoniambia, alisema, "Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa." Vema, kama ni kwa kanisa, kanisa hilo ni lipi? Katoliki, upande mmoja, kuna Katoliki ya Kirumi inayosema, "Sisi ndio," Katoliki ya Kiyunani inasema, "Ni sisi." Na loo, jamani, awamu tofauti—tofauti za Katoliki, ni ipi kati ya hizo iliyo sahihi? Mnaona?

52 Kisha unasema, "Vema . . . " Ndipo Mlutheri anasema, "Sisi ndio kanisa," Mbaptisti anasema, "Sisi ndio kanisa," Mmethodisti anasema, "Sisi ndio kanisa," Mpentekoste anasema, "Sisi ndio kanisa." Ninii—ninii . . . Vema, kuna madhehebu mia tisa na sitini mbalimbali, basi kanisa ni lipi? Ingetatiza sana. Mnaona? Lakini Mungu atawahukumu watu kwa Neno Lake, maana hilo ndilo Neno.

53 Sasa, katika Kitabu cha Ufunuo, lilisema, "Atakayeondoa lolote katika hiki Kitabu, ama kuongeza lolote Kwake, huyo ataninii, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima." Sasa, ninaamini ni kamilifu sana, kwamba sababu ya sisi kupatwa na mauti siku hizi, huzuni, magonjwa, maeneo haya ya makaburi hapa nje, kila mtu aliyewahi kufa, kila mtoto mchanga anayeteseka, kila ugonjwa ulikuwa ni kwa sababu Hawa alikosa kuamini kwamba Neno la Mungu lilitosha, hakuliamini Neno la Mungu, na hiyo ikasababisha mauti.

54 Mungu alilipa Kanisa Lake, Mungu hawezi kubadilika, kwa hivyo Mungu alilipa Kanisa Lake Kitu kilicho bora zaidi, na Mungu anapofanya uamuzi kamwe hawezi kusema, "Nilikosea." Mnaona? Je, mnalielewa? Tazama. Mungu . . . Labda ninazungumza kwa sauti kubwa sana, na—natumai sifanyi hivyo, mimi . . . Mungu hawezi kamwe kubadili uamuzi Wake. Ninaposema chochote, au ukisema chochote, sisi tuna kikomo, hiyo inamaanisha ni binadamu tu. Nasi husema, "Mwaka ujao tutajifunza mengi kuliko tuliyojua mwaka uliopita." Mimi—mimi . . . Mnaona, ni—ninakuwa mwerevu zaidi, unakuwa, kila mmoja wetu huwa hivyo, lakini sio Mungu. Yeye hana kikomo, hiyo ina maana kwanza kabisa Yeye ni mkamilifu. Kila uamuzi ni mkamilifu, Yeye hawezi kamwe kubadilisha Wake.

55 Angalieni, msije mkaelewa vibaya, katika bustani ya Edeni, wakati mwanadamu alipotenda dhambi kwanza na kukata ushirika, akajitenga na Mungu, ushirika na Mungu, sasa alijaribu kujiundia mwenyewe dini, akashona majani kadhaa

apate kujifunika. Lakini dini yake ya kujibunia isingefanya kazi, ndipo Mungu akafanya uamuzi wa toleo la damu, akaua wanyama, akachukua ngozi na kuwafunika.

56 Sasa, huo ulikuwa ndio uamuzi wa Mungu, katika bustani ya Edeni, kumwokoa mwanadamu na kushirikiana na mwanadamu kupitia damu iliyomwagika ya kiumbe kisicho na hatia, wala Yeye hajawahi kuubadilisha. Kamwe hatutaweza kufikia mahali, tuseme, "Sisi sote lazima tuwe Walutheri; sote lazima tuwe Wakatoliki; sote lazima tuwe *hiki* au *kile*." Lakini mahali pamoja Mungu hukutana na mwanadamu, na hapo ni juu ya msingi wa Damu iliyomwagika, Damu ya Yesu Kristo, Mwanawe. Ilikuwa hivyo mwanzoni.

57 Katika Israeli, mwanadamu alikutana tu . . . Mungu alikutana tu na mwanadamu chini ya damu iliyomwagika, katika siku za Ayubu, damu iliyomwagika tu. Kote katika historia imekuwa ni damu iliyomwagika, kwa sababu hiyo ilikuwa ndiyo utambulisho wa kwanza wa Mungu kwa mwanadamu, jinsi ya kumwokoa, kwa damu.

58 Mnaona, wakati Mungu anapotenda kazi, anapoitwa jukwaani kutenda, sasa, msisahau jambo hili, wakati Mungu anapoitwa wakati mmoja . . . jukwaani kutenda kazi, jinsi Yeye anavyotenda mara ya kwanza, kila wakati tukio hi—hilo linapoibuka tena, au kisa chochote kama hicho, Yeye hana budi kutenda jinsi alivyotenda mara ya kwanza, la sivyo Yeye alitenda vibaya alipotenda mara ya kwanza. Sasa, mnaelewa dhahiri kabisa? Rafiki zangu Wahindi wanaelewa hilo dhahiri kabisa?

59 Angalieni, kwa maneno mengine, ikiwa—ikiwa mtu alitenda dhambi, naye Mungu akasema, "Nita—nitamwokoa chini ya damu iliyomwagika," hiyo ni . . . Sasa, halafu mtu mwingine aje, Yeye hana budi kumwokoa pia, mtu mwingine, mtu mwingine, na kila mtu. Na basi kama mtu ni mgonjwa, na Mungu alimponya mtu wa kwanza kwa msingi wa imani yake katika Mungu, hivyo ndivyo Mungu alivyomponya mtu wa kwanza, na sasa kila mtu anayekuja baadaye, Yeye, kwa imani akiamini, Mungu hana budi kufanya jambo lile lile. Kama hakufanya hivyo, alitenda vibaya kwa mtu wa kwanza. Sasa, mnajua ninachomaanisha? Alikosea alipotenda kwanza. Mnaona? Kwa hiyo hana budi kutenda vivyo hivyo kila wakati.

60 Sasa, mnasema, "Naam, sasa, labda hili halikumaanisha hivyo." Kamwe usiamini hilo. Kila Neno alilolinena Mungu analimaanisha Milele. Unaona? Neno ni Mungu, unaona, kwa hiyo haliwezi kushindwa.

Sasa, unasema vema, "Naam, haileti tofauti yoyote." Naam, inaleta, enyi marafiki.

61 Sasa angalieni, wakati Lutu alipoitwa kutoka Sodoma, ninyi watu mnakumbuka hadithi hiyo? Hakika. Sasa, Malaika

alimwambia Lutu na mkewe, familia yake, "Msiangalie nyuma." Na sasa, mwazieni mama huyo, mke wa Lutu, watoto wake walikuwa wakiteketea, huko chini, katika Hukumu za Mungu, wajukuu wake walikuwa wakiteketea katika Hukumu za Mungu. Naye aligeuza tu kichwa chake kutazama nyuma, naye anasimama pale, hata wa leo, kama nguzo ya chumvi. Tunajua hilo. Mnaona? Inaleta tofauti. Mungu anaposema chochote, anamaanisha kile anachosema. Sasa, ni wangapi katika jengo hili, Wahindi na wazungu pia, wanaoamini ya kwamba Mungu anamaanisha kile hasa asemacho, kwamba Yeye—Yeye kawezi kubadilika, anamaanisha kile asemacho? Vema.

62 Sasa—sasa, kabla hatujalikaribia Neno Lake, nami nataka. . .Nitawazungumzia kidogo tu juu ya Neno. Sasa, hatutaliacha Neno kamwe. Tunapaswa kudumu. . .Ninaamini Neno. Mungu anaweza kufanya mambo mengi ambayo hajayaandika katika Biblia Yake. Lakini maadamu mimi. . . Nikimwona tu akifanya yale aliyoandika, hayo yanitosha. Mwache tu. . .Sawa tu namna hiyo. Ni—ninaamini hivyo, basi tunajua tuko sahihi.

63 Sasa, kwa ndugu zangu wahudumu hapa, makasisi, ili kwamba. . .Wao ni nanii wenu. . .Hao ni wachungaji wenu. Sasa, katika Agano la Kale, Mungu alikuwa na njia ya kujua, au, watu walikuwa na njia ya kujua kama ujumbe ulikuwa sahihi au la. Sasa, nabii alipotabiri, au mwotaji aliota ndoto, walimpeleka hekaluni, kulikokuwa na kile kifuko cha kifuani cha Haruni ambacho kilikuwa na hayo mawe yote ya kifuani, kumi na mawili, na hapo nabii huyu alipotabiri akiegemea jiwe hilo, au mwotaji alipoisimulia ndoto yake, kama (Hiyo inaitwa Urimu na Thumimu.), basi kama taa hizo hazikumulika juu ya hiyo Urimu na Thumimu, basi, haidhuru inasikika halisi jinsi gani, haikuwa sahihi. Ilibidi Urimu na Thumimu inene kama ilikuwa sahihi au si sahihi. Mnajua hilo, ndugu. Hiyo ni kweli. Vema sasa, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya ukuhani wa Walawi. Sasa, yale Mungu aliyofanya pale. . .Sasa, Yeye kamwe habadiliki, kumbukeni, Yeye hawezi kubadilika, hana budi kudumu.

64 Yesu, alipokuja, Yeye alisema, "Mmewasikia watu wa kale, 'Usiue,' lakini Mimi nasema kwamba kila amkasirikiaye ndugu yake bila sababu amekwisha kuua." Je, hiyo ni kweli? Sasa, mnaona, Yeye kamwe—Yeye kamwe hakuibadilisha, aliikuza tu, akaifanya kuwa kubwa zaidi. Mnaona?

65 Akasema, "Mmewasikia watu wa kale, 'Usizini,'" ilibidi awe katika hicho kitendo apate kuwa na hatia, akasema, "lakini mimi nawaambia, ya kwamba kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Mnaona? Aliitoa kutoka kwenye tendo halisi hadi kwenye tamaa ya hilo tendo, mnaona, akaikuza zaidi.

66 Sasa, wakati Urimu na Thumimu, kutoka kwenye kile kifuko cha kifuani cha Haruni, ilipobadilishwa, ililetwa kwenye Neno, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Mnaona? Basi lazima iwe kulingana na Neno.

67 Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, kwa maombi, nasi tu—tutamkaribia Yeye. Sasa, katika mkesha tu wa mkutano huu wa siku tatu usiku pamoja nanyi watu wapendwa, nashangaa miongoni mwenu, usiku wa leo, kuna haja ambayo ungependa ikumbukwe mbele za Mungu, ukisema hivi, "Mungu, Wewe unaujua moyo wangu, nina kitu ninachohitaji, nitainua mkono wangu. Basi, Mungu, kabla mkutano huu haujaisha, mkutano huu wa siku tatu usiku, nipe uponyaji wa mwili wangu, au kwa dada yangu, kwa ndugu yangu, kwa—kwa mama yangu, baba, au kwa wokovu," au chochote unachohitaji.

68 Kama una haja kama hiyo, je, waweza tu kumwinulia Mungu mkono wako? Acha tu ijulikane, unapoinua mkono wako, useme, "Mungu, nikumbuke." Sawa. Sasa, na tuombe.

69 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi cha neema, tusingekuja kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu, Kiti cha Enzi cha haki, tusingeweza kusimama hapo, kwani hakika hatupaswi kuwa na haki ya kuja, kwa maana tulikuwa wenye dhambi. Lakini tumekuja kwenye Kiti cha Enzi cha neema, ambacho ulitwambia tuna haki za kuja.

70 Na sasa, Baba wa Mbinguni, unajua ninii . . . yaliyo nyuma ya mikono hii iliyoinuliwa. Chini yake kulikuwa na moyo, na katika moyo huo kulikuwa na haja. Mungu, jalia kwamba kabla ya siku hizi tatu usiku kupita, kila moja itajibiwa. Tujalie, Bwana. Waokoe waliopotea, waponye wagonjwa, Bwana.

71 Sasa, tunajua ya kwamba ulijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwako sisi tuliponywa. Sasa, tunatambua, Baba wa Mbinguni, ya kwamba ulipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, basi kila dhambi ulimwenguni ilisamehewa, lakini haitatusaidia kamwe, mpaka tumkubali Yeye kama Mwokozi wetu kutoka katika dhambi hiyo. Lakini suala la dhambi limetatuliwa wakati Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alipokufa kuiondoa dhambi ya ulimwengu.

72 Nasi tunafundishwa kwamba kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Sasa, tunajua kwamba uponyaji tayari umekwisha tatuliwa machoni pa Mungu, kwa sababu Mwanawe Mwenyewe alipigwa kwa ajili ya uponyaji wetu, "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Nasi tunajua kwamba tunaweza kukubali uponyaji tunapoamini, kama vile tu tunavyoukubali wokovu.

73 Sasa, Baba, je, utakuja kati yetu na kutujulisha kwamba umefufuka katika wafu, kwamba unaishi leo, na uko . . . Wewe, ungali unabaki Yesu yeye yule mwenye upendo, na kwamba wakati unakaribia . . . ?[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .

tukiiangalia dunia kwenye matukio haya yajayo, Wewe ulisema huo ulikuwa ndio wakati wa kuinua kichwa, kwa maana ukombozi wetu unakaribia.

74 Nabii alitwambia kutakuwa na siku ambayo isingeweza kuitwa usiku wala mchana, ingekuwa siku ya utusitusi, ukungu mwingi, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru. Nalo jua lile lile linalochomoza mashariki ni lile lile linalotua magharibi, j-u-a lile lile linalovuka anga. Naye M-w-a-n-a wa Mungu aliyekuja mashariki na kumwaga Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho, wakati wa jioni, huku kwenye Pwani ya Magharibi, ameondoa ukungu na kumwaga Roho Mtakatifu apate kutoa Nuru ya jioni, kama tu alivyoahidi. Tunakushukuru kwa ajili yake, Baba.

75 Sasa, mimi niko hapa juu miongoni mwa wageni wa . . . watu hawa wa thamani wanaoishi hapa, tukikutazamia Kuja kwa Bwana. Sasa, tunaomba ya kwamba utajitukuza Mwenyewe mbele yetu, kwa njia ambayo tutajua ya kwamba Wewe uko hapa.

76 Na tunapoondoka, usiku wa leo, kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, siku ile baada ya ufufuo . . . Ulitembea pamoja nao siku nzima, wala hawakukujua Wewe. Ndipo ulipokutana nao wakati wa jioni, na ukawaingiza ndani na kuifunga milango, basi ulifanya jambo fulani kama ulivyolifanya kabla hujasulubiwa, nao walijua hakuna mtu angeweza kufanya jambo hilo kama Wewe, na huyo alikuwa ni Wewe. Basi wakakimbia huko, na kusema, "Kweli, Bwana amefufuka. Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, alipokuwa akizungumza nasi njiani?" Tujalie, Bwana, usiku wa leo, tunapoenda nyumbani mwetu.

Jalia tumwone Bwana Yesu aliyefufuka, papa hapa katika jengo hili, akiwaponya wagonjwa, na akionyesha rehema kwa wote. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

77 Sasa, huku katika Biblia ya kale iliyobarikiwa, na kwa ajili ya somo tu . . . Na sasa, ninawatakeni msikilize kwa makini sana sasa, nami nitachukua tu wakati wangu na kujaribu kueleza hili vizuri zaidi niwezavyo. Sasa, kama utalishika hili kwa karibu sana . . .

78 Sasa, marafiki zangu wote wa Kihindi wanajua Kiingereza. Hiyo ni kweli? Wote wanaweza kuzungumza Kiingereza? Vema. Kila mtu hapa ndani anazungumza Kiingereza, Wanorwe, na kadhalika? Mnaona, nawatakeni . . . Kweli, nilitaka kusema kama hawakukifahamu, ningekuwa na mtu wa kuja kutafsiri, maana sitaki mlikose hili.

79 Sasa, nyinyi ni wasikilizaji wazuri sana, ningeweza tu kusimama na kuzungumza kwa saa kadhaa, na—nami na—nawapenda kwa sababu najua mnampenda Bwana wetu.

80 Sasa, ninataka kusoma sehemu mbili kutoka kwenye Maandiko. Na mojawapo inapatikana katika Yohana Mtakatifu 12:20, mlango wa 12 na kifungu cha 20, hayo mengine ndiyo kiini cha uamsho wetu, Waebrania 13:8.

81 Sasa, huu ni ujumbe mdogo rasmi tu ambao kwa kawaida tunatanguliza ibada, na kisha tutawaombea wagonjwa. Ndipo basi kesho, labda, mtaelewa vizuri zaidi. Kumbukeni kuja kanisani mapema.

82 Na sasa, kutakuwa na mvulana hapa, mwanangu, ama Ndugu Eddie, ama Ndugu Roy, ama baadhi yao, mtu fulani atakuwa hapa na kadi za maombi. Nao wanaleta kadi hizi za maombi mbele zenu, wanazichanganya zote pamoja, na kushuka na kumpa kila mtu kadi ya maombi, ili kwamba mvulana anayezichanganya, hatakuwa na uhusiano wowote kwamba ni kadi gani ya maombi inayotolewa.

83 Halafu ninapokuja mkutanoni, hatujui kamwe mstari wa maombi utaanzia wapi. Tunaweza kuanzia kwenye hamsini, tunaweza kuanzia kwenye ishirini, tunaweza kuanzia kwenye kumi, tunaweza kuanzia kwenye moja, tunaweza kuanzia mia moja na kurudi nyuma, vyovyote tu. Mtu yeyote aliyewahi kuhudhuria mikutano (ninyi ndugu, nadhani mmewahi), mnajua ya kwamba hiyo ni kweli. Kwa hiyo basi si lazima uwe na kadi ya maombi, ikiwa tu una imani. Kwa kawaida kuna takriban watu kumi kwenye kusanyiko wanaoponywa ambapo mmoja anaponywa jukwaani. Unakuwa tu na imani na kuamini.

84 Sasa, Yohana Mtakatifu, mlango wa 12, kifungu cha 20:

> *Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida . . ., wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

Sasa, katika Waebrania 13:8, ilisema:

> *Yesu Kristo ni yeye yule jana, . . . leo na hata milele.*

85 Sasa, nitafanya somo kutokana na hayo na kusema hivi: *Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu*. Sasa, ni wangapi wangependa kumwona? Hebu tuone mikono yenu. Ni wangapi tu sasa? Asanteni kwa shauku yenu ya kumwona Bwana wetu.

86 Sasa, kama nilivyowaambia, ninaamini Biblia ni Neno la Mungu, na lazima iwe vile Mungu asemavyo hasa, na Yeye hana budi kutimiza kila ahadi, la sivyo si Neno la Mungu. Angalieni, kama ni . . . kama hiyo . . . Kama hatatimiza ahadi Yake, basi si Neno la Mungu. Mungu asingeweza kuwa Mungu, atoe ahadi kisha asiitimize. Mnaona? La, la. Huyo angekuwa ni mwanadamu. Hicho kingekuwa ni kitabu cha kujibunia. Lakini Kitabu cha Mungu ni Neno la Mungu.

87 Sasa, sasa, Wayunani hawa walikuwa wamesikia habari za Yesu, lakini hawakuwa wamemwona Yesu. Ndipo wakaja kwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu, ambaye jina lake lilikuwa Filipo, mwenyeji wa Bethsaida katika Galilaya, na kusema, "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Sasa, yeye alikuwa mtumishi wa Yesu, kwa hiyo akampeleka mbele ya Yesu, na kumwonyesha Yesu.

88 Sasa, Biblia ilisema hapa, Paulo akiandika katika Waebrania 13:8, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele. Je, nyote mnaamini hilo? Sawa.

89 Sasa, kama hao Wayunani walitaka kumwona Yesu, nanyi mnataka kumwona Yesu, na mmoja wa watumishi wa Mungu aliwachukua na kuwaonyesha Yesu, na ikiwa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa nini mtumishi wa Mungu asiweze kuwaonyesha Yeye leo kama Yeye ni yule yule?

"Vema," mnasema, "lakini alikufa."

90 Naam, lakini alifufuka tena. Mnaona? Hajafa. Yu hai. Mnaona? Yeye hajafa, Yu hai. Sasa, mwili Wake wa kawaida, huo ni mwili, ulitwaliwa juu mbele za Mungu, umeketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Naye Roho Mtakatifu akarudi chini, ambaye alikuwa ni Roho wa Kristo, naye anaishi ndani ya Kanisa. Mnaamini hilo, sivyo? Sasa, kama tungeuliza swali hili, "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu?" na sasa ikiwa Yesu, ninii . . .

91 Mimi, nikiwa mmishenari, ninasafiri kila mahali ulimwenguni. Nami nilikuwa tu huko Bombay, India, hapa si muda mrefu uliopita, ambako nilikaribishwa katika hekalu la Wajaini, dini ya Jaini. Basi kulikuwa na dini kumi na saba mbalimbali zilizowakilishwa katika hekalu lile, alasiri hiyo, wapate kuzungumza nami, na kila mmoja wao aliupinga Ukristo.

92 Sasa, wazia hilo, wanaabudu sanamu, wanyama, na baadhi yao wanaamini katika kuzaliwa upya kama kiumbe mwingine, yaani, unakufa kitu kimoja na kurudi kingine. Ilikuwa ni mchafuko mbaya sana uliowahi kuona, lakini wakati Bwana wetu Yesu alipokuja jukwaani, hilo lilitosha. Nilichukua andiko lili hili mbele ya watu mia tano elfu usiku huo, hao ni watu nusu milioni wakiketi katika uwanja mkubwa mno wa michezo, ukumbi wa michezo, kitu kama hicho, na kuchukua andiko lile lile, ambapo Waislamu, na Wabudha, Makalasinga, Wajaini, loo jamani, wa kila namna ungaliweza kuwazia, na Maraja wakiwa wamekalia mito ya hariri. Meya wa Durban alikuwepo, na—na mvulana wa Mahatma Gandhi alikuwepo, na—na, loo, wengi sana.

93 Na hapo, wakati Roho Mtakatifu alipoanza kuwafunulia hao watu . . . Ndipo basi, akaja mtu . . . Nao walidhani ilikuwa ni telepathia. Ndipo akaja kipofu jukwaani, akiwa na kadi yake ya

maombi, mtu wa nne. Nami nikaona ono ya kwamba ataponywa, nami nikatoa changamoto kwa kila dini iliyokuwako, iyafungue macho yake.

94 Nikasema, "Kama hii ni telepathia, njoni mkayafungue macho yake." Nikasema, "Basi mbona hamji? Kuhani wa Kiislamu, mbona usije?" Nikasema, "Unafikiri . . . nisingefanya chochote . . . Nisingesema hivyo kwa chochote, ningeogopa kusema, lakini nimeona ono hivi punde kwamba amefunguliwa macho. Sasa, asipofunguliwa macho, basi mimi ni nabii wa uongo, kama akifunguliwa macho, ni wangapi watamkubali Kristo kama Mwokozi?" Bahari tu ya mikono!

95 Nikasema, "Njoo hapa, bwana." Ndipo ikamwambia alikuwa ninii . . . amekuwa kipofu kwa miaka *kadhaa*, naye alikuwa ombaomba, na kadhalika, na yote kuhusu alikuwa na watoto wangapi, na kwa hiyo hiyo ilikuwa ni kweli, lakini bado waliamini ilikuwa ni telepathia, kama kusoma akili. Mnaona?

96 Na kwa hiyo, nikasema, "Sasa, kusoma akili, ni . . . Sijui lolote kuhusu saikolojia." Nikasema . . . Na mtu yeyote anayejua saikolojia kamwe hangeita hiyo saikolojia. Hivyo basi wao . . . Nikasema, "Sasa, kama hivyo ndivyo, ninyi maprofesa wa saikolojia njoni hapa mkayafungue macho yake." Lilikuwa ni kundi nyamavu sana.

97 Nikasema—nikasema, "Nyinyi Waislamu ndio dini kubwa sana duniani." Hiyo ni kweli. Kuna Waislamu wengi kuliko wote. Nami nikasema, "Kwa nini makuhani wenu wasije hapa na kuyafungua macho yake?" Nikasema, "Vipi kuhusu nyinyi Wabudha?" Budha aliishi kama miaka elfu mbili mia tatu iliyopita, mwanafalsafa wa Kichina . . ., au, mwanafalsafa wa Kijapani. Nikasema, "Sasa, kwa nini msije mkayafungue macho yake?" Nikasema, "Nilikuwa kwenye hekalu la Wajaini alasiri ya leo. Kuna na—nanii," kama papa, "kiongozi wao mkuu, njoo, umfungue macho, nitajiunga na dini yako." Hakuna aliyesema lolote.

98 Nikasema, "Mna shida gani?" Mnaona? Nikasema, "Sasa, kama hii ni telepathia, basi njoni, ninyi ndio mabingwa wake, si mimi, njoni, myafungue macho yake." Mnaona? Nikasema, "Kama Mwislamu ni . . . Mtu fulani hana budi kuwa sahihi, na mtu mwingine hana budi kuwa makosani, hatuwezi sote kuwa sahihi." Hiyo ni kweli.

99 Nikasema, "Mungu ambaye ni Mungu wa uumbaji na amuumbie macho, ndipo tutajua kama ni kweli au la." Nami nikasema, "Nisingesema hivyo kama sikuwa nimeona tayari alikuwa anaenda kufunguliwa macho yake." Lakini nikasema, "Yeye yuko, na kama hafanyi hivyo, basi mnifukuze kutoka India, mimi ni nabii wa uongo, kama akifanya hivyo, ninyi mpokeeni."

100 Nikamwashiria aje pale. Mara nilipoomba, akapiga mayowe, angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza, kama mtu yeyote yule. Hakika. Ndipo basi, iliwabidi kuninii . . . Hata nisingeweza kutoka nje ya jengo, na mambo kama hayo. Iliwabidi kuninii . . . Hata walikuwa na wanamgambo pale, loo, nadhani askari elfu moja mia tano, mia sita kabla sijapata kufika kwenye gari, saa mbili baadaye. Na . . .

101 Lakini ni nini, marafiki? Mungu, kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Na kama Yeye si Mungu yule yule, basi kuna kasoro fulani, kwanza kabisa asingeweza kuwa Mungu. Kwa hiyo . . . Mnaona? Kwa hiyo Yeye hana—Yeye hana—Yeye hana budi kubaki vile vile.

Sasa, sasa, kama tungesema, "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu . . . " Sasa, kama ningewaambia Walutheri hapa usiku wa leo, "Mnawaziaje juu yake?"

102 "Loo, hakika, ninaamini Yeye ni yeye yule." Wabaptisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, Wakatoliki, wowote wale, yote ingekuwa, "Naam, Yeye yuko kanisani mwetu, na . . . tunaye. Sisi . . . Huyu ni wetu. Yeye—Yeye ni Mungu wetu. Yu—Yuko pamoja nasi."

103 Vema sasa, ninaamini hilo pia, nitaamini hilo pamoja nanyi. Lakini sasa, ngojeni kidogo, kuna njia moja tu ya kulifanya jambo hilo kuwa sahihi, kuna njia moja tu ya kujua yakini, ni kutafuta kujua kile alichokuwa jana. Mnaona? Chochote alichokuwa jana, hana budi kuwa vivyo hivyo leo. Je, hiyo ni kweli? Mnaona, si kama . . .

104 Sasa, tusingeshuka kwenda mjini kutafuta mtu, tuangalie huku na huku . . . Tungesema, "Yesu Kristo yuko pamoja nasi." Tusingeshuka kwenda katikati mwa jiji kumwona mtu aliyevaa joho, na makovu ya misumari kichwani mwake, ama, alama za miiba, na makovu ya misumari mkononi mwake, mnafiki yeyote angeweza kufanya hivyo. Mnaona, mnaona? Inahitaji Uhai ndani yake kufanya jambo hilo, mnaona, Uhai Wake, Uhai wa huyo Mtu.

105 Yesu alisema hapa katika Yohana Mtakatifu, "Yeye aniaminiye Mimi, ninii," Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Maana Uhai Wake . . . Kama tungekuwa, mti wa mwenye dhambi na Mti wa Kristo uwekwe ndani yetu, basi Uhai huo ungezaa matunda, hasa tu kama vile mpichi kwa mpera, ama kadhalika, mtofaa, kwa chochote ulichokuwa. Hiyo ni kweli? Mnaona, ingebidi uone kile Yeye alichokuwa jana.

106 Sasa, Paulo akizungumza hapa alikuwa anazungumza juu ya jana, maana yake Agano la Kale. Alichokuwa jana ndicho alicho leo, na atakuwa milele. Hilo ni Agano la Kale, Agano Jipya, na hata milele, yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona?

107 Sasa, Yeye alikuwa nini jana? Sasa, kama alikuwa ninii—kama alikuwa mtu mashuhuri, tajiri jana, angekuwa mtu mashuhuri, tajiri leo. Lakini alipokuja jana, tunaona ya kwamba hata hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Hiyo ni kweli. "Ndege wa angani wana viota, mbweha wana mapango; lakini sina hata mahali pa kulaza kichwa Changu."

108 Yeye—Yeye alikuwa na . . . Alipokuja ulimwenguni, aliazima tumbo la uzazi apate kuzaliwa, hawakuwa na kitanda cha kumlaza, kwa hiyo wakamlaza katika sanduku la majani. Alipokufa, alitundikwa kwenye mti wa Kirumi chini ya adhabu ya kifo. Alikuwa na vazi moja la kuvaa, alikuwa ameshonewa, "limefumwa bila mshono." Ilimbidi kuazima kaburi la kuzikiwa. Kwa hiyo hakuna hata mmoja wetu aliye fukara hivyo.

109 Alikuja kuonyesha kile alichokuwa Mungu. Chochote chenye majivuno na kiburi si Mungu. Mungu ni mpole na mnyenyekevu, hiyo ndiyo iliyomfanya Mungu. Mnaona, kitu kinachojidhili, si wale wanaojikweza. Kwa hiyo Mungu hakai katika matabaka, na kadhalika, Yeye huishi katika unyenyekevu. Njia ya kupanda ni kushuka. "Jidhili nawe utakwezwa; jikweze nawe utadhiliwa." Hiyo ni kweli. Unaona? Mungu anajua jinsi ya kufanya hivyo. Kwa hiyo huna budi kukumbuka, jinyenyekeze mbele za Mungu. Usijaribu kuwaza mawazo yako mwenyewe, yawaze mawazo Yake. Unaona?

110 Na silaha zote za Mkristo, sasa, hazionekani. Mkristo huangalia kile ambacho haoni, kimaumbile. Sasa angalieni, hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kuwa Mkristo. Huna budi kumwamini Mungu, Yule usiyeweza kumwona. Mnaona, sasa tazama. Tazama hapa. Silaha zote za Kikristo ni upendo, furaha, imani, uvumilivu, subira, upole, unyenyekevu, Roho Mtakatifu. Mnaona? Mambo hayo yote ni yasiyoonekana, hayaonekani. Lakini mambo yasiyoonekana ndiyo yaliyo na uhalisi, mambo yasiyoonekana.

111 Sasa, tutamchukua Yesu. Sote tunajua kuzaliwa Kwake, jinsi alivyobashiriwa tangu bustani ya Edeni, "Uzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka, naye atamponda kisigino," na kadhalika.

112 Sasa, lakini alipokuja, alizaliwa horini, Naye akalelewa katika nyumba duni, kisha akaenda kuishi pamoja na watu fulani, Martha, Mariamu, na Lazaro. Ndipo kwenye umri wa miaka thelathini, Yohana Mbatizaji akambatiza katika mto Yordani, ndipo Mungu akashuka, katika umbo la Roho Mtakatifu . . . katika Roho Mtakatifu katika umbo la hua, akaingia ndani Yake, na kukaa ndani Yake.

113 Sasa kumbukeni, "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Je, hiyo ni kweli? Vema. "Sio Mimi," kasema Yesu, "nizifanyaye hizo kazi, bali Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo

kazi." Sasa, kama mnaandika Maandiko, Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda lolote Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Sasa, kumbukeni, si yale *anayomsikia* Baba akisema, bali yale *amwonayo* Baba akiyatenda.

114 Kwa hiyo, Yesu hakufanya lolote mpaka Mungu alipomwonyesha, kwa ono, la kufanya kwanza. Kama hakufanya hivyo, Maandiko yamekosea. Yohana Mtakatifu 5:19 ilisema, "Amin, nawaambia," hilo linamaanisha kabisa, "Nawaambia, Mwana hawezi kutenda lolote kwa nafsi Yake, ila lile amwonalo Baba akilitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile. Kwa maana Baba anatenda kazi, nami ninatenda kazi vile vile." Kwa maneno mengine, Yeye aliigiza tu katika mchezo wa kuigiza kile ambacho Mungu Baba, alimwonyesha kufanya, maana Mungu alikuwa ndani ya Kristo.

115 Sasa, Mathayo 3, ilisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa," alipokuwa anashuka, Sauti ikinena kutoka kwa Huyo, Mungu, aliyekuwa akishuka, kama hua, Yohana alishuhudia kumwona, Ndipo Sauti ikatoka Kwake, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ndani Yake, ambaye ninapendezwa kukaa *ndani* Yake." Na kama ningeifanya hivi kusudi mpate kuelewa vizuri zaidi, ambapo wafasiri wa mwanzoni katika King James . . . Kama ukichukua Kiyunani asilia, inasema hivi: "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Lakini mnaona, ni jambo lile lile. "Ninayependezwa kukaa ndani Yake." Mnaona? "Ninapendezwa kukaa ndani ya Mwanangu." Ndipo akawa Imanueli, Mungu pamoja nasi.

116 Sasa, sasa, sasa, Yohana Mtakatifu, nilisoma kutoka kwenu, Yohana Mtakatifu 12:20. Sasa, hebu turudi kwenye Yohana Mtakatifu, na tuanze, na tukae tu katika Yohana Mtakatifu, usiku wa leo, tukionyesha kile yalicho Maandiko katika Yohana Mtakatifu kumhusu Yeye. Sasa, tutaona kama tunaweza kujua kile Yeye alichokuwa, usiku wa leo, kesho usiku tutaingia kwenye kilindi chake zaidi kidogo, na kesho kutwa usiku, tuendelee tu.

117 Angalieni sasa. Yohana Mtakatifu, hebu . . . Tulisoma mlango wa 12, hebu turudi na tusome mlango wa kwanza sasa, alisema sasa, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Sasa, mnaweza kulipata? "Hapo mwanzo alikuwako Neno."

118 Sasa, *neno* ni nini? *Neno* ni "wazo lililotamkwa." Inakubidi kuliwazia kabla ya kulitamka. Mnaona? Na, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na kama Neno liliwahi kuwa Mungu, bado ni Mungu. Mnaliona? "Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, "Neno

alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu . . . ” Neno la Mungu lilifanyika mwili miongoni mwetu katika Kristo Yesu. Mnaamini hilo? Yeye alikuwa Neno la Mungu lililofanyika mwili.

119 Sasa, naye Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, pia katika mlango wa 10 na kifungu cha 37, Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Kwa maneno mengine, kile ambacho Baba alikuwa amedhihirisha kwamba Yeye alikuwa, kama hakufanya hicho, basi msimwamini; hiyo ni busara tu. Mnaona?

120 Na katika Yohana Mtakatifu 5:39, ilisema, "Yachunguzeni Maandiko; kwa maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia." Kwa maneno mengine, Yeye alikuwa Neno lililo hai, Yeye alikuwa Neno la Mungu lililodhihirishwa. Loo, jinsi ninavyopenda ku—kuingia katika jambo hilo: Neno la Mungu likidhihirishwa, kwa maneno mengine, likifanywa lijulikane, Neno la Mungu likifanywa lijulikane. Kwa maneno mengine, Yeye Ndiye ambaye Mungu aliishi ndani yake ili kufanya Neno Lake lijulikane.

121 Kristo alionyesha kile ambacho Neno lilifundisha. Amina. Haya basi. Kristo alikuwa Dhihirisho la Neno lililoandikwa; Kristo alilidhihirisha. Si ajabu Yeye aliwaambia hao Mafarisayo, viongozi wa kidini wa siku Zake, Yeye alisema, "Enyi wanafiki," kasema, "jua likitua dhahiri, mnasema kesho kutakuwa na kianga. Kama ni kwekundu na kumetanda, mnasema kutakuwa na dhoruba." Kasema, "Mnaweza kuutambua uso wa mbingu; lakini ishara ya wakati hamwezi kuitambua. Kwa maana kama mngelinijua Mimi, mngeliijua siku Yangu." Mnaona?

122 Walikuwa na dini, loo, jamani, nyingi sana. Lakini walikosa kumwona Yeye kama Masihi, kwa sababu . . . Sasa, mnajua Yeye hakuja kwa njia mbaya; alikuja jinsi hasa Neno lilivyotabiri, bali si kulingana na yale waliyokuwa wakiwazia, walikuwa nalo kwa njia nyingine. Lakini Yeye alikuja vile hasa Biblia ilivyotabiri Yeye angekuja, ila tu, walikuwa wameifasiri Biblia vibaya.

123 Nashangaa kama inaweza kuwa hivyo tena. Hapana shaka ila ambapo kuna—kuna tafsiri nyingi sana tofauti Zake. Kwa hiyo mnaweza kuona, hapana shaka kuna kasoro mahali fulani. Baadhi yao wanasema, "Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," wengine wanasema, "Siku za miujiza zimepita. Roho Mtakatifu aliwashukia tu wale mitume kumi na wawili," na—na wengine wanasema jambo moja, lazima kuwe na kitu cha kweli na cha uongo mahali fulani. Hiyo ni kweli.

124 Pia kumbukeni, kabla ya kuwa na . . . Ikiwa una dola bandia, hiyo ni dola ghushi, kabla ya dola hiyo ghushi kutengenezwa, lazima kuwe na dola halisi ambayo imetengenezwa kutokana nayo, kama sivyo, ndiyo ya asili. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . lazima kuwe na dini halisi ambayo hiyo imeundwa

kutokana nayo. Kweli kabisa. Kila moja yazo ilianza kwenye Pentekoste, bali walipitia tu njia tofauti na kuliacha Neno.

125 Na hiyo ndiyo sababu. . . Siku hizi, tunawezaje kumtarajia Mungu kutenda kazi, na kulirudisha kanisa kwenye lile Tukio la Kipentekoste, huku tunakana ukweli wenyewe kwamba Yeye hufanya jambo hilo?

126 Kama ambavyo nimesema mara nyingi, "Ni. . . Ingefaa nini kumlisha kurumbizi vitamini C nzuri, kufanya mabawa makubwa, yenye nguvu na manyoya mazuri, na kisha kumweka kwenye kizimba?" Haingefaa kitu, sivyo? Bila shaka haingefaa kitu. Iwapo utamlisha vitamini, na kuimarisha mbawa zake, mwachilie tu, acha aruke. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya. Tunahitaji kurumbizi wanaoruka. Hiyo ni kweli. Achilieni, na mambo hayo tunayoamini kumhusu Mungu, tumieni imani hiyo. Bila shaka, bila shaka. Tunaamini hilo. Usimfunge huko nyuma, useme, "Hasha, siku za miujiza zimepita." La, hazijapita. Zimepita kwa wale wanaoamini kuwa zimepita, lakini kwa wale wanaojua vizuri zaidi, ni tofauti. Naam.

127 Jamaa fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, akasema, "Sijali unachosema, ni watu wangapi unaotaka kutoa," kasema, "bado siamini katika uponyaji wa Kiungu. La, bwana."

128 Nikasema, "Bila shaka huamini. Haikuwa kwa ajili ya wasioamini, ilikuwa ni kwa ajili ya waumini pekee." Hivyo tu. Hivyo tu. Ni kwa wale tu wanaoamini, hivyo tu.

129 Sasa, tunamwona Yesu, sasa, amekuja kudhihirisha Neno. Sasa, hilo Ndilo alilokuwa jana, hilo Ndilo Yeye alilo leo hii, hilo Ndilo atakalokuwa milele: Neno la Mungu lililodhihirishwa. Je, hilo ni neno bora zaidi? Liwazieni, huh? Neno la Mungu lililodhihirishwa, ikaonyesha ya kwamba ni Kweli. Na kila kitu ambacho Mungu alisema angefanya, alikifanya. Kila kitu kilichoandikwa katika Biblia kwamba atafanya, Yeye alikifanya, kweli kabisa, kwa maana Yeye alikuwa Neno lililodhihirishwa.

130 Vema, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na ahadi hizi zote zikining'inia kwa kizazi hiki, kwa nini asiwe yule yule leo kudhihirisha kila kitu ambacho Neno la Mungu liliahidi? Mnaona? Haina budi kuwa, ni yeye yule kabisa, maana Hilo ndilo alilokuwa wakati huo, Hilo ndilo Yeye alilo sasa, Hilo ndilo atakalokuwa milele: Neno la Mungu likidhihirishwa. Amina. Hata katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu moja bado atakuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Loo, jinsi hilo linavyopaswa kuwasha imani yetu, mnaona, kujua ya kwamba iko pale. Na kama Yeye ni Roho Mtakatifu kuliangazia Neno hilo. . .

131 Sasa, Neno ni Mbegu. Sasa, wengi wenu ndugu, mlio—mlio hapa, nadhani, hulima. Nawe uweke mbegu ardhini, na kesho yake asubuhi utoke uende na kuichimbua, na kusema, "Mahindi yangu hayakui bado," uirudishe, uifunike. Kesho yake asubuhi,

"Mimi . . . Nitaona kama inakua tena." Kamwe haitakua hivyo. La, la. Kila unapoichimbua, unaichelewesha. Hiyo ni kweli?

132 Unafanya nini? Unajua ardhi iliumbwa ipate kukuza mahindi (Hiyo ni kweli?), ama, ninii—ama mbe—mbegu. Nawe unapanda mbegu, unaitia ardhini, na kusahau habari zake, Mungu anafanya yaliyosalia. Vema, hivyo ndivyo unavyofanya na Neno la Mungu, unalipanda tu, usilichimbue. Endelea tu kuliamini, na kulikabidhi kwa Mungu, Yeye hulifanya likue. Hiyo ni kweli. Unaona?

133 Ahadi yoyote ambayo Mungu anatoa, wewe ninii tu—wewe ipande tu moyoni mwako na kusema, "Ni yangu, Mungu alinipa." Unaona? Sasa, unaweza usione matokeo yoyote kwa sasa. Kamwe hukuyaona mazao yako ya mahindi, mara tu ulipopanda mahindi yako, lakini kwa uwezekano yapo. Maadamu hutayasumbua, na uendelee kuyanyunyizia maji, yata—yatakua. Usijali kuhusu hilo, itachukua, ikiwa ni mbegu iliyorutubishwa. Na kila Neno la Mungu limerutubishwa na Mungu Mwenyewe. Mungu yuko katika Neno, kwa hiyo litakua, unajua litakua.

134 Haya basi. Inatubidi kulichukua Neno Lake, kulikubali, kuliamini, kulikabidhi, Nalo linakua. Hiyo ni kweli. Lakini usiendelee kulichimbua sasa, utaliharibu. Utaharibu mazao yako kila wakati unapofanya hivyo. Kwa hiyo likabidhi tu kwa Mungu na uamini.

135 Sasa, kwa mfano kama, tuseme kwa mfano, nilikuwa hapa juu ya mlima mahali fulani, nimetupwa na sikuwa na chakula. Na kabla sijaweza kupata chakula chochote . . . Mkate mmoja ungeyaokoa maisha yangu, na bei ya kununua huo mkate, tuseme, senti ishirini na tano. Vema, ningesema . . .

Mtu fulani aingie, na kusema, "Kuna nini, Ndugu Branham?"

"Ninakufa njaa, nitakufa."

"Kwa nini?"

"Sina mkate."

Vema, unasema, "Kwa nini usiende ununue mkate?"

"Sina pesa."

"Vema, mkate mmoja ni senti ishirini na tano."

"Naam, bwana, lakini sina senti ishirini na tano." Unaona?

Vema, ungesema, "Hapa, Ndugu Branham, chukua senti hizi ishirini na tano ukajinunulie mkate."

136 Loo jamani, ningeninii tu—ningecheza tu yosayosa kidogo pande zote. Kwa nini? Ninaweza kufurahi tu nikiwa na robo mkononi mwangu, kununua mkate, kama vile ningefurahi nikiwa na mkate, kwa sababu ninao uwezo wa kununua mkate.

137 Ni kama tu, ile *pale* duka, yote ninayopaswa kufanya ni kuiweka chini, na kuuchukua mkate. Kwa hiyo ninaweza tu kufurahia nikiwa na hiyo robo mkononi mwangu kama vile ningefurahi nikiwa na mkate, kwa sababu ni uwezo wa kununua huo mkate.

138 Kwa hivyo ushahidi wa uponyaji wako ni nini unapoamini? Haijalishi ni nini kitakachotokea, unasema, "Sijisikii vizuri zaidi, sininii . . ." *Hakina* uhusiano wowote nayo. Una uwezo wa kununua, unaamini. Kwa hivyo anza tu kucheza yosayosa kidogo, ukisema, "Mungu asifiwe, nitakuwa mzima, kwa sababu nina uwezo wa kununua mkate huo." Haya basi. Unaona?

139 Sasa, hakuna mtu anayeweza kukuponya, kwa maana tayari umeponywa. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Biblia inafundisha hilo. Tayari umeponywa, "Kwa kupigwa kwake uliponywa." Unaona? Sasa, hakuna mtu anayeweza kukuponya. Wala huwezi . . . Kama Yesu angesimama hapa Mwenyewe, hangeweza kukuponya, tayari ameshafanya hivyo. Unaona? Hiyo ni kweli kabisa. Ingekubidi kuamini hilo.

140 Sasa, wakati alipodhihirishwa na tukaona kile Yeye alichokuwa jana, hebu na tuliendeleze mbele kidogo. Sasa, tunajua ya kwamba manabii wa Agano la Kale, Mungu daima alikuwa na watu Wake wa kuwaamini manabii Wake. Tunajua hilo, sivyo? Kwa sababu Biblia ilisema ya kwamba Neno la Mungu, Neno sasa ambalo lilikuwa ni Mungu, liliwajia manabii. Hiyo ni kweli? Neno la Bwana liliwajia manabii; Neno la Bwana lilimjia Yeremia; Neno la Bwana lilimjia Musa; Neno la Bwana lilikuja kwa njia tofauti kwa manabii, ndio waliokuwa na Neno la Mungu. Nao, kwa kuwa Nalo walilidhihirisha. Mnaona? Wanalidhihirisha, kwa sababu liliwajia. Walikuwa Nalo, wakalinena, wakasema yale hasa yangetukia, nayo yakatukia. Na hivyo ndivyo walivyojua wao walikuwa manabii. Sasa, mnalipata?

141 Mnaona? Neno lilimjia nabii, sehemu, si Lote, sehemu Yake tu ingemjia nabii. Naye angedhihirisha jinsi Neno lilivyokuwa hasa, nalo lilitimia jinsi tu alivyolisema.

142 Naye Mungu akasema, "Ikiwa kuna mtu miongoni mwenu aliye wa kiroho au nabii, Mimi, Bwana, nitajidhihirisha Mwenyewe kwake katika maono, nitasema naye kwa ndoto. Na kama nabii huyu akitabiri, na yale asemayo yatimie, basi msikieni nabii huyo, kwa kuwa Mimi niko pamoja naye." Hilo ni Neno ndani yake. Mnalipata? "Lakini kama akitoa unabii, wala hautimii, basi msimwogope nabii huyo, maana mimi siko pamoja naye."

143 Lakini mnaona, kama likitimia, basi hiyo ilithibitisha ya kwamba ilikuwa ni Neno la Mungu ndani ya huyo nabii. Alisema, na ikawa. Sasa, wao daima walipaswa kuwaamini manabii wao.

144 Sasa, katika Kumbukumbu la Torati, mlango wa 18, Musa, ambaye aliwapa Israeli torati, alisema . . . aliwaambia kuhusu wakati wa mwisho. Naye akasema, "Bwana Mungu wenu atawainulia miongoni mwenu, kutoka kwa ndugu zenu, Nabii kama nilivyo mimi. Na itakuwa kwamba, yeyote ambaye hatamsikia Nabii huyo atakatiliwa mbali na watu." Sasa, vile . . . Ndipo tunajua ya kwamba alikuwa akizungumza juu ya Masihi, maana kote kote, hata walimwuliza Yohana, "Wewe Ndiwe yule Nabii? Wewe ndiwe yule Nabii?" Wakaendelea kusema, "Wewe ndiwe yule Nabii?" Mnaona? Maana walijua ya kwamba huyo Nabii alikuwa anakuja.

145 Sasa, nabii wa mwisho wa Agano la Kale alikuwa Malaki, miaka mia nne na kitu kabla ya Kuja kwa Kristo. Ndipo mara ghafla, Kristo anajitokeza jukwaani, Naye anabatizwa katika Yordani na Yohana. Baba anashuka chini katika mfano wa Roho Mtakatifu, anaingia ndani Yake. Huyo anaenda nyikani, kujaribiwa na ibilisi siku arobaini, kisha anarudi akiwa na huduma Yake. Hebu tuangalie kile Yeye alichokuwa sasa, mnaona? Sasa tunaona kile Yeye alichokuwa. Kile alichokuwa ndani ya manabii, tuliona. Sasa, tutaona kile Yeye alicho . . . kile alichokuwa jana, ndipo sisi, kama Paulo alivyosema, leo hii, kisha tuone kile atakachokuwa milele. Mnaona?

146 Sasa, huyu hapa anatoka. Jambo la kwanza tunalomwona akifanya . . . Kulikuwa na mtu jina lake Simoni, naye alikuwa na ndugu jina lake Andrea. Naye Andrea alikuwa akihudhuria mkutano wa Yohana, naye, Yohana, akasema, "Huyo hapo Mwana-Kondoo wa Mungu, aondoaye dhambi ya ulimwengu." Naye Andrea akaenda pamoja Naye, naye alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi. Basi akaja, akamwambia Simoni, ndugu yake mvuvi, tunayemjua kwa jina la Petro, akamwambia, kasema, "Nimempata Masihi. Njoo, umwone."

147 Sasa naweza kuwazia . . . Hebu tulichambue tu, tuone yale hapana shaka Simoni aliwazia. Alisema, "Sasa, ngoja kidogo hapa. Sasa, mimi ni msomaji wa Biblia. Baba yangu mzee, kabla hajafa, aliniambia, 'Mwanangu, kutakuwa na kila kitu kabla ya Masihi kuja.'" Kwa sababu sikuzote kuna lundo la waongo wanaoinuka kupingana na—na yaliyo kweli, tunajua hilo, nyakati zote. "Sasa, yeye alisema, 'Sasa, kutakuwa na watu wa kila namna wanaotaka kuwa Masihi.'" Na huyo ni Yesu, Mwokozi. "Kasema, 'Kutakuwa na wengi wao,' lakini akasema, 'usidanganyike, dumu na Neno, kwa kuwa Masihi huyo atakuwa yule Mfalme-Nabii. Mtamjua kwa sababu atafanya ishara ya nabii. Unaona? Kwa maana Musa, Maandiko yetu, alitwambia ya kwamba Masihi ambaye atainuliwa miongoni mwetu atakuwa nabii kama yeye. Neno la Mungu litakuwa pamoja Naye, atakuwa akidhihirisha Neno la Mungu.'" Amina.

148 Mnalipata? Neno la Bwana litakuwa pamoja naye, maana Yeye atakuwa nabii, Naye atakuwa akidhihirisha Ne—Neno la Bwana.

149 Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo yananishuhudia Mimi. Nami kama sizitendi hizo kazi, basi msiniamini Mimi. Lakini kama hamwezi kuniamini Mimi, nikiwa Mwanadamu, aminini kazi nizifanyazo, mpate kuokolewa." Mnaona? Kamilifu!

150 Sasa, walikuwa wakimtazamia Nabii huyu ainuke. Ndipo wakati. . .Bila shaka Andrea aliingia mbio, kamwambia. Loo, huenda aliwazia, "Andrea, umerukwa na akili."

151 Kwa hiyo, siku moja, alishuka akaenda kumwona Yesu ufukoni. Ndipo wakati alipoenda Mbele za Yesu, sasa, kumbukeni Simoni, jina lake lilikuwa Simoni wakati huo, bali alipoenda Mbele za Yesu kwa mara ya kwanza, Yesu kamwe hakuwa amemwona, sasa mwangalie Yeye sasa, mara alipoingia Uweponi Mwake, Yesu alimtazama huku na huku na kusema, "Jina lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona."

152 Loo, jamani! Hilo lilimpata. Loo, hakujua tu kwamba yeye alikuwa ni nani, bali alimjua huyo baba yake mzee mtauwa. Kwa hiyo huyo hapo Nabii, hakuna mtu angeweza kulikana, huyo hapo, akifanya vivyo hivyo kabisa. Alimjua, na alimjua baba yake. Akasema, "Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona. Nami nitakuita. . .Tangu sasa, nitakuita Petro," ambalo linamaanisha "jiwe dogo, maungamo," kwa sababu Petro alimkiri.

153 Sasa, kulikuwa na mtu aliyesimama pale jina la—lake Filipo, yule ambaye tumesoma habari zake hivi punde akimpeleka mtu huyu kwa Yesu, aliona hilo naye akawazia, "Aisee, hilo latosha, kwa sababu Biblia ilisema ya kwamba Masihi huyo angekuwa nabii. Naye Huyu hapa, tunamwona."

154 Kwa hiyo alikuwa na rafiki ambaye alisoma naye Biblia, yale magombo ya kale, nalo jina lake lilikuwa Nathanaeli. Kwa hivyo kutoka mahali ambapo Yesu alikuwa akihubiria, kama ukipata kwenda kule, ni maili kumi na tano kuzunguka mlima hapa kufikia ambapo Nathanaeli aliishi. Kwa hiyo Filipo aliondoka akatimua mbio kuzunguka hapa, siku hiyo. Ndipo kesho yake asubuhi akakutana na Nathanaeli bustanini akiomba, akasema, "Njoo, umwone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

155 Vema, yeye. . .Walikuwa wamejifunza Maandiko pamoja tangu ujanani, wakahudhuria kanisa moja, naye akasema, "Sasa, ngoja kidogo hapa, ngoja kidogo. Je, kunaweza lolote jema kutoka Nazareti?"

Akasema, "Njoo, uone."

"Je, kitu kama Hicho kinaweza kutokea . . .?"

156 Sasa, hilo ni—hilo ni jibu zuri kwa mtu yeyote, "Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, ujionee." Hilo bado ni zuri leo. "Njoo, ujionee mwenyewe."

157 Hawa hapa wanapiga kona, wakija huku, akasema, "Sasa, angalia. Je, unamkumbuka yule mzee aitwaye Simoni, ambaye hangeweza kuandika jina lake, wakati wewe . . . yeye . . . alinunua samaki kutoka kwako, wala asingeweza kukupa . . . asingeweza kutoa risiti?"

"Loo, naam. Yule mwana wa Yona?"

158 "Naam. Jana alikuja mbele ya Masihi, ambaye tunamjua, Masihi. Hakuwa amewahi kumwona maishani mwake mwote. Naye akasema, 'Tazama, jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.' Sasa tazama, sote wawili tunayajua Maandiko. Na je, Biblia yetu haituambii kwamba Masihi angekuwa nabii? Naye Huyu hapa, akifanya hivi."

159 Aah, Filipo asingeweza kuamini hilo, ama, Nathanaeli. Kwa hiyo akaja Mbele za Yesu, basi alipoenda Mbele za Yesu, Yesu alimwangalia moja kwa moja na kusema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" kwa maneno mengine, mtu mwenye haki.

160 Nalo likamstaajabisha, akasema, "Rabi," inamaanisha "mwalimu," "Rabi, ulinijua lini Wewe? Hujawahi kuniona. Mbona, ni—ninatoka sehemu nyingine ya nchi, ndiyo kwanza nije hapa. Hujawahi kuniona, unajuaje mimi ni mtu mwenye haki?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Ni macho ya jinsi gani!

161 Mnajua kile huyo msomi wa Biblia alichosema? Alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli." Kwa nini? Aliona Yeye alikuwa dhihirisho kamili la Neno la Mungu. Miaka mia nne bila nabii naye Huyu hapa amesimama, yale hasa Biblia ilisema angefanya. "Rabi, Mwalimu, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli."

Yesu akasema, "Kwa sababu nilikwambia hivi unaamini? Basi njoo, unifuate Mimi, utaona makuu kuliko haya, unaona."

Vema. Loo, huyo alikuwa ni Yesu jana.

162 Sasa, kuna jamii tatu tu za watu ulimwenguni kote, iwapo tunaiamini Biblia. Loo, najua wanadai kuna nyingi, lakini angalieni, sote tulitokea, baada ya yale maangamizi yaliyoitangulia gharika, wakati ulimwengu ulipoharibiwa kwa maji, tunaamini kwamba kama Wakristo, Nuhu alikuwa na wana watatu, Hamu, Shemu, na Yafethi, nasi sote tulitoka kwa hao wavulana watatu, hapana shaka.

163 Na sasa, kama ukiangalia, Petro alipewa funguo za Ufalme, na hizo zilikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Sasa, Petro alikuwa na funguo za Ufalme. Kwenye siku ya Pentekoste, aliifungua Injili kwa Wayahudi, Matendo 7, akawafungulia Wasamaria, Filipo alishuka akawahubiria Wasamaria, ila tu hawakuwa . . . waliamini, ila walikuwa tu wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, ndipo akashuka na kuwawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Kisha katika Matendo 10:49, alifungua Injili kwa Mataifa kwenye nyumba ya Kornelio. Mnaona? Kunao watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Mmelipata? Hizo jamii tatu.

164 Sasa, kulikuweko na hizo jamii mbili zikimtazamia Masihi, hizo zilikuwa ni Myahudi na Msamaria. Lakini sisi Waanglo-Sakson, Wamataifa, tuliabudu sanamu, rungu mgongoni mwetu, nasi tuliabudu sanamu, hatukuwa tunamtazamia Masihi. Naye kamwe hakufanya hivyo mbele ya Masihi yeyote, ah, la, hiyo ishara hapo mbele ya Mmataifa yeyote, kamwe, haijaandikwa katika Neno. Lakini angalieni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake iliyothibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

165 Waangalie hawa Wayahudi shupavu, Petro, na (Ni nani mwingine tunayeweza kusema?) wengi wao, yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu aliyeligusa vazi Lake, Zakayo, juu ya mti, Bartimayo kipofu, imani yake ilimsimamisha, Naye akageuka, Wayahudi hawa wote shupavu. Yeye alionyesha kwamba alikuwa Masihi kwa kuwa Nabii aliyejidhihirisha Mwenyewe.

166 Sasa, sasa, tunaona . . . Tunawachukua wawili. Tutachukua tu . . . sasa, tutaondoka . . . tutarudi kesho usiku, tuwachukue Wayahudi wengine. Lakini sasa, usiku wa leo, tutamwendea Mmataifa, ama, Msamaria, hiyo hapo jamii nyingine inayomtarajia Masihi. Sasa, wakati Yeye yuko duniani, hana budi kujidhihirisha Mwenyewe kwa wale wanaomtazamia, hana budi.

167 Angalieni. Sasa, hapa Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi, kwa njia gani? Kunena siri za moyo wao, kuwaambia yale waliyokuwa wamefanya, na kadhalika, tunajua hilo. Sasa, je, hiyo ilithibitisha Yeye alikuwa Neno? Ni wangapi wanaamini hilo?

168 Sasa, mnayaandika Maandiko, andikeni hili. Waebrania, mlango wa 4, yapata kifungu cha 12, ilisema, "Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya mfupa na mafuta, nalo ni Mtambuzi wa mawazo ya moyoni." Hiyo ni kweli, ndugu? Neno la Mungu huyatambua mawazo yaliyo mioyoni mwao. Aliwatazama na kuyatambua mawazo yao. Hiyo ni kweli? Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Neno. "Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo." Hiyo ndiyo sababu walijua

ya kwamba Yeye alikuwa dhihirisho la Neno la Mungu; huyo alikuwa ni Yesu jana.

169 Sasa, Yeye alikuwa akienda zake Yeriko. Yerusalemu iko juu ya kilima, Yeriko iko bondeni. Alikuwa anaenda Yeriko, lakini alikuwa na haja ya kupitia Samaria, sasa, huo ni m—mji wa Sikari. Akasimama, akawatuma wanafunzi Wake waingie wakanunue chakula, hapana shaka ilikuwa yapata wakati wa adhuhuri.

170 Walipokuwa wameondoka, kulikuwa na mwanamke mrembo aliyejitokeza hapo, alikuwa mwenye sifa mbaya, tunajua unachomaanisha hapo, wa namna ya ukahaba, lakini huenda alikuwa ni msichana wa kupendeza. Hapana shaka ila kwamba alikuwa msichana wa kupendeza, lakini labda alikuwa na kitu kilichosababisha hilo, labda mama yake alimwingiza mtaani alipokuwa mtoto.

171 Mwajua, tunazungumza sana huku Marekani kuhusu kutowajibika kwa vijana, si kutowajibika kwa vijana, ni kutowajibika kwa wazazi. Wakati mwingine msichana huenda mrama kwa sababu mama yake hamfanyi atende mema. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hivyo mara nyingi ni kosa la wazazi, sio watoto, kutowajibika kwa vijana.

172 Kwa hiyo hapa tunamkuta huyu msichana mdogo, alitokea, yeye ni mwanamke kijana, labda katika miaka yake ya ishirini ya mwanzoni. Akajitokeza…Sasa, nimekuwa katika nchi za mashariki, ninazijua hizo mila, kamwe hazibadiliki. Sasa, sababu ya yeye kutokwenda mapema, pamoja na wanawali, kisimani, kuteka maji, hakuruhusiwa, hawashiriki pamoja, na kwa hiyo, ilimbidi kwenda baadaye; kwa hiyo huyu hapa anatoka karibu adhuhuri.

173 Na mnapaswa kuona jinsi wanavyoyabeba maji. Wana ninii kubwa mno…Si, sio ndoo, ni ninii—ni chungu cha udongo. Ni ninii…kinabeba kama galoni tatu, nadhani, nacho kina mpini juu yake. Na halafu, wana kisima chenye winchi, nao wanachukua kulabu hizi na kuzitumbukiza katika mitungi hii mikubwa, na kuishusha, na kuijaza maji, na kuivuta juu kwa winchi.

174 Nami nimeona wasichana wadogo, la, vema, wasichana wadogo tu wameketi na kuweka moja ya vyungu hivyo vikubwa vya maji juu ya kichwa chake, kimoja kwenye kila bega, na kundi zima lao wakienda zao wakipiga gumzo, wakitikisa vichwa vyao, wakisemezana, hawamwagi hata tone, kamwe. Jinsi wanavyolifanya, sijui. Wangali wanafanya hivyo, wanazungumza, kama tu kina mama wawezavyo, mwajua. Kwa hiyo wanaenda huko wakizungumza tu na kamwe wasimwage maji hata kidogo, na wangali wanafanya hivyo.

175 Sasa, alitoka kwenda kuteka chungu chake cha maji, naye akaanza kukishusha. Sasa, kisima hicho, bado kingali pale, ni

ninii tu . . . ndicho ambacho Yakobo alimpa Yusufu, mwanawe. Na kwa hiyo, ilikuwa ni mandhari kidogo, karibu kama jukwaa hili hapa juu. Na hii . . . Na kuna ukuta uliozunguka, halafu kisima cha umma pale ambapo watu hunywea. Kwa hiyo akaanza kuteremsha ndoo ndani, ama, chungu, ndipo akamsikia Mtu fulani akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Naye akageuka na kuangalia.

176 Sasa, Yeye hakuwa ila, na yapata umri wa miaka thelathini na mitatu, bali alionekana ana zaidi ya hamsini. Mnajua Biblia ilisema hivyo? Um-hum. Katika Yohana Mtakatifu 6 aliposema, "Mimi ndimi Mkate wa Uzima utokao kwa Mungu Mbinguni. Baba zenu walikula mana nyikani, nao wamekufa." Akasema, "Lakini Mimi ndimi Mkate wa Uzima utokao kwa Mungu Mbinguni. Mtu akila Mkate huu hatakufa kamwe." Loo, waliendelea kujadiliana kwa muda kidogo.

177 Na hivyo, basi wao . . . Yeye akasema . . . Akawaambia. Kasema kwamba, "Unasema wewe, umemwona Ibrahimu, wakati hujapata zaidi ya umri wa miaka hamsini?" Alikuwa na thelathini tu, lakini kazi Yake hapana shaka ilimfanya aonekane hamsini. "Wewe si mtu wa zaidi ya miaka hamsini, nawe wasema kwamba ulimwona Ibrahimu?" Kasema, "Sasa, tunajua una pepo, nawe una wazimu, kichaa." Unaona?

Akasema, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Hilo lilitosha.

Naye Huyu hapa sasa, karibu, ki—ki—kijana Myahudi aliyeketi pale akiangalia tu. Na hivyo, akasema, "Nipe maji ninywe."

178 Naye akasema, "Sio kawaida," walikuwa na ubaguzi wakati huo kama tulivyokuwa nao huko kusini, mwajua, kati ya watu weusi na weupe. Kasema, "Sio kawaida kwako, ukiwa Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria . . . chochote," kasema, "hatuna uhusiano wowote."

Akasema, "Mwanamke, kama ungejua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe, nami nikupe Maji ambayo huji hapa kuchota."

Akasema, "Kisima ni kirefu," unaona, bado ni mawazo ya kimwili. "Kisima ni kirefu," kisha kasema, "huna kitu cha kuchotea."

Akasema, "Maji nitoayo ni Uzima wa milele, yakibubujika."

179 Wana ninii . . . ? . . . Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiwasiliana na roho yake. Mnaona? Kuwasiliana. Alipopata shida yake ilikuwa ni nini . . . Ni wangapi wanaojua shida yake ilikuwa nini? Alikuwa na waume watano, alikuwa akiishi na wa sita. Akasema, "Mwanamke, nenda kamwite mumeo, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Kasema, "Umesema kweli." Kasema, "Una watano... umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye wako, hapo umesema kweli."

180 Sasa, angalieni, wakati alipofanya jambo hilo mbele ya hao Wayahudi, hao Wayahudi walisema, hao makuhani wakuu, na walimu wa siku hizo, kasema, "Ahem." Iliwabidi kujibu kanisa lao. Lilikuwa likitukia, kwa hiyo iliwabidi kuwaambia kusanyiko lao jambo fulani, wasingeweza kulikwepa, maana iliwabidi kukabiliana na suala hilo.

181 Kwa hiyo akasema, "Ahem." Kasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli, mkuu wa pepo," mpiga ramli, kwa maneno mengine. Kasema, "Yeye ni mpiga ramli." Na mtu yeyote anajua mpiga ramli ni wa ibilisi. Kwa hiyo akasema—akasema, "Yeye ni Beelzebuli, yule mpiga ramli." Vema.

182 Basi alipofanya hivyo, akageuka, akawatazama hao Wayahudi, akasema, "Nitawasamehe, Mimi, Mwana wa Adamu, nitawasamehe kwa kusema hivi, kulikufuru Neno la Mungu. Lakini," kasema, "siku moja," kwa maneno mengine, "Roho Mtakatifu anakuja kufanya kazi iyo hiyo, na neno moja dhidi Yake mtu hatasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao."

183 Kwa hivyo mnaona mahali linapotuweka. Neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe. Huko ni kumkufuru Roho Mtakatifu. Walipomwona amesimama pale pamoja na wale... Yeye alikuwa Neno, nalo Neno lilikuwa likijieleza Lenyewe kama tu Biblia ilivyosema, nao wakasema, "Yeye ni mpiga ramli." Nanyi mnajua kilichowapata, kila mmoja wao alipotea. Kweli kabisa.

Sasa, Huyu hapa amesimama pamoja na mwanamke huyu, Naye akasema, "Nenda kamwite mume wako."

Mwanamke akasema, "Sina yeyote."

Akasema, "Umesema vema. Umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye wako."

184 Yeye...Ati nini? Mwangalie maskini huyu kahaba, Akageuka, akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Ni tofauti jinsi gani! Mwanamke huyo alijua zaidi kuhusu Mungu kuliko nusu ya wahubiri nchini Marekani, hiyo ni kweli, katika hali yake.

185 Angalieni, alisema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sisi," Wasamaria, "tunajua kwamba yuaja Masihi, aitwaye Kristo. Na atakapokuja, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake." Loo, jamani! Hicho ndicho alichokuwa jana. Mnaona? Mnaona? "Tunajua ya kwamba Masihi, aitwaye Kristo, atakapokuja atatwambia mambo haya. U nani Wewe?"

Naye akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

186 Basi alifanya nini? Aliacha mtungi huo wa maji, akakimbilia mjini, naye akasema, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

187 Na watu katika mji huo wakamwamini kwa sababu yule mwanamke alisema ya kwamba Yeye alimwambia aliyoyafanya. Hiyo ni kweli? Vema, huyo alikuwa ni Yesu jana. Sasa, haikuwa ni vazi Lake, wote walivalia sawa. Haikuwa vile Yeye alivyoweka ndevu Zake, ama kuchana nywele Zake, wote walizichana vile vile. Bali ilikuwa ni dhihirisho la Neno la Mungu ndani Yake, likiyatambua mawazo ya moyo. Ni wangapi wanaamini hilo?

188 Vema, huyo ni Yesu jana; huyo angekuwa Yesu leo, sivyo? Yesu yeye yule, Yesu yeye yule aliyekuwa pamoja na Musa, Musa aliondoka Misri, akihesabu shutuma la Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko ule wa Misri. Huyo alikuwa ni Yesu jana. Paulo alisema, “Ni yeye yule leo na atakuwa hivyo milele.” Ni kwa nini? Yesu ni Neno, Dhihirisho la Neno, Neno lililofanyika mwili.

189 Sasa, katika kufunga ninaweza kusema hivi. Tungeweza kusimama hapa usiku kucha, lakini hatufiki mwisho wake, maana ni Biblia nzima tu, imekumbatiwa tu pale pale. Mnaona? Sasa, kumbukeni. Huo ulikuwa ndio mwisho wa kipindi cha Kiyahudi, na—na Wasamaria, huo—huo ulivimaliza.

190 Sasa, wakiwa watatu, hao walikuwa watu wa Hamu na Shemu. Sasa, vipi kuhusu watu wa Yafethi, watu hawa, Mataifa? Sasa, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Nao walikuwa na miaka elfu nne ya kuamini Yeye alikuwa anakuja. Naye alipokuja, hawakumwamini. Ndipo akafanya ishara ya Kimasihi kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, nao Wayahudi waliokusudiwa Uzima wakaliamini.

191 Mwangalie maskini huyo kahaba. Vema, angelikaa nje ya makanisa yao, pengine rasmi, baridi, na yamekauka, hayakumfaa hata kidogo. Lakini ni . . . yeye alichaguliwa tangu zamani kwa Uzima wa Milele. Na mara tu jambo hilo lilipofanywa, upesi akalitambua. Ilikuwa ni nini? Hiyo Nuru . . . Hiyo Mbegu ikachipukia Uzima. Naam. “Wote alionipa Baba watakuja. Wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Amina. Haya basi.

192 Na mara hiyo Nuru ilipoangaza, alisema nini? Kasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua yuaja Masihi kufanya jambo hili. Na atakapokuja . . . ”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

193 Sasa, haikuwa sawa kwake kwenda mjini, lakini hebu jaribu kumzuia. Haijalishi alikuwa nini, hebu jaribu kumzuia wakati mmoja. Ni kama kuzima nyumba, nayo inaungua moto siku yenye upepo. Loo, alikuwa na ushuhuda. Alijua Neno, naye akasema, “Huyo hapo Masihi pale, Yeye aliniambia mambo

ambayo nimefanya. Yachunguze Maandiko. Haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?"

194 Nao hao watu wakasema, "Ndilo hilo," nao wakamwamini. Hakufanya hivyo tena, Yeye alimfanyia tu mwanamke huyo mmoja, akamwonyesha jambo hilo. Nao watu wote wa mjini wakamwamini Yesu kwa sababu yule mwanamke alisema hivyo. Loo, jamani!

195 Sasa, Yeye hakufanya miujiza yoyote kule. Aliondoka, kwa maana alijua Filipo alikuwa akishuka mumo humo kufanya miujiza moja kwa moja nyuma Yake. Mnaona? Kwa hiyo Yeye aliliacha tu hilo hivyo, akaenda zake. Walijua huyo alikuwa ni Masihi. Hiyo ilitosha. Miujiza ingefanyika maadamu unamtambua Masihi.

196 Sasa, tazama. Sasa, tumekuwa na miaka elfu mbili ya theolojia, kama vile Wayahudi walivyokuwa na miaka elfu nne. Mungu, kutoka kwa Mataifa, atawachukua wa—watu kwa ajili ya Jina Lake. Mnaamini hilo? Vema.

197 Sasa je, mnaamini tuko kwenye wakati wa jioni? Sasa, angalieni yale Yesu aliyosema hapa. Nitanukuu kutoka kwako. . .kutoka kwa Luka 17:28. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," sasa, nafunga, "katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Ni wangapi waliowahi kusoma hilo? "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu." Sasa, hali—haliwezi kushindwa, alisema. Mnaona? Sasa, angalieni.

198 Sasa, Yeye aliendelea mbele na kusema habari za Nuhu, jinsi walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, na utovu wa uadilifu wake. Na kisha akasema, "Vivyo hivyo, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake."

199 Angalieni. Katika siku za Sodoma. . .Sasa, ngojea. Kulikuwa na mtu aliyeitwa kwa uteuzi, Ibrahimu. Alikuwa mtu wa kawaida tu, Mungu alimwita alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano, na. . .alikuwa na sabini na mitano, na mke wake alikuwa na sitini na mitano, na akamwambia watapata mtoto. Naye aliamini Neno hilo kwa muda wa miaka ishirini na mitano, naye alikuwa na mia moja, naye mke wake alikuwa na tisini, ndipo huyo mtoto mchanga akaja.

200 Laiti ningekuwa na wakati wa kupitia somo hilo dogo pamoja nanyi kwa takriban wiki moja hapa. Loo, jamani! Ninaamini ya kwamba imani ya Kihindi ingelipuka moja kwa moja kutoka juu ya ile maskani pale, mnaona, kuliweka hilo wazi.

201 Nimepitia Grass Valley kule chini hivi punde kwenye. . . Loo, jamani! Na huko Grass Valley, ambako kanda na kadhalika zilikuwa zimechezwa, kabla ya kuja, nami nikachukua hiyo,

sikumwombea mtu yeyote, nikaiacha tu, na kuichukua hiyo na kuuelezea Uzao huo wa Ibrahimu, na imani ya Ibrahimu, na Uzao wa Ibrahimu . . .

202 Si kwamba tu Mungu alimwahidi Ibrahimu, bali na Uzao wake baada yake. Nasi ni Uzao wa Ibrahimu, nasi tuko ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Kifalme wa ile ahadi. Naye Ibrahimu alifanya nini? "Kuviita vitu ambavyo havikuwako kana kwamba vilikuwako, kwa sababu Mungu alisema hivyo." Jamani! Ninaweza kuona, wakati Mungu alipomwambia, alisema, "Ibrahimu, utapata mtoto kwa mke wako."

203 Sasa, kumbukeni, sitini na mitano amekoma hedhi kwa yapata miaka kumi na mitano, ishirini, mabadiliko ya maisha. Mnaona? Sasa, alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na minane, hakukuwako na mtoto. Alikuwa tasa . . . Mke alikuwa mgumba, yeye alikuwa tasa, hana mtoto, na hata hivyo, Mungu alisema, "Utampata." Basi, "Ibrahimu hakusita kwa ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimsifu Mungu." Hiyo ni kweli.

204 Vipi kuhusu watoto wake? Huo ulikuwa ni uzao wa kimwili. Vipi kuhusu Uzao wa Kifalme kupitia Kristo, kwa imani ile ile aliyopokea ya kumpata? Amina. Loo, jamani! Hilo lingekubeba likupeleke huko mbali kupita mwezi, na nyota, na kukuendesha kwenye Njia ya Kilimia Cheupe, naam, bwana, kupita Jupita, Zuhura, na Mirihi, na kuendelea, kwenye imani hiyo, unaona, imani ya Ibrahimu. Angalieni.

205 Ninaweza kumwona Ibrahimu akisema, akija nyumbani kutoka kondeni, aseme, "Mpenzi, jitayarishe, tutapata mtoto." Ungeweza kuwazia mzee, umri wa miaka sabini na mitano, mkewe sitini na mitano, wakishuka kwenda kwa daktari, waseme, "Dak, hebu nikwambie kitu, naomba ujitayarishe, tutapata mtoto. Tunataka kuandaa chumba cha hospitali."

Daktari angesema, "Loo, loo. Naam, bwana. Uh-huh," na kuwapigia polisi simu haraka sana wakamchukue, amerukwa na akili. Mnaona? Mnaona?

206 Mtu yeyote, anayelichukua Neno la Mungu, anayeamini Neno la Mungu, kidogo anahesabiwa kuwa na kichaa, mwajua. Ndivyo walivyo, kwa sababu wamepoteza nia ya ulimwengu, wana nia ya Mungu. Mnaona?

207 "Andaa vitu." Vema, basi, siku ishirini na nane za kwanza zikapita, na sasa, jinsi maskini Sara alivyoandaa vijibuti, mnajua, na kuandaa vijibuti vyote, kisha akachukua jicho ndege, na vipini, na kila kitu, akaviandaa. Kwa hiyo atapata mtoto, hakika kabisa, ndipo basi siku ishirini na nane zikapita.

Kasema, "Wajisikiaje, mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, utapata mtoto kwa vyovyote vile."

Sasa . . . ? . . . wanasema, "Aha! Nilidhani hutampata."

208 Mungu alisema, "Jitenge na hao wasioamini. Njoo huku katika nchi nyingine, ukatembee pamoja Nami." Loo, jamani! "Waondokeeni maskini hao wasioamini, wa—watawadhuru. Tokeni miongoni mwao." Hiyo ni kweli. Tokeni miongoni mwao, hawataki kuamini.

Mwaka wa—wa kwanza ukapita, Ibrahimu akajongea na kusema, "Sara, mpenzi, unajisikiaje?"

"Hakuna tofauti, mpenzi."

"Utukufu kwa Mungu, huyo mtoto ni mwujiza wa mwaka mmoja zaidi. Haleluya! Tutampata kwa vyovyote vile. Weka hivyo vijibuti tayari."

Naam, takriban miaka kumi, kumi na mitano, labda miaka ishirini ikapita, akasema, "Ibrahimu, mpenzi, vijibuti hivi vinachakaa."

"Jifumie vingine vipya. Haleluya! Tutampata kwa vyovyote vile."

"Vema, lakini, Ibrahimu, sijisikii tofauti hata kidogo."

"Si kile unachohisi, Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Tutampata kwa vyovyote vile, Mungu alisema hivyo." Loo, ndugu. Loo, jamani!

Sasa, ana umri wa miaka mia moja, loo jamani, naye Sarah ana tisini, maskini bikizee, mwajua. "Unajisikiaje, mpenzi?"

"Hakuna tofauti, mpenzi."

"Haleluya! Tutampata kwa vyovyote vile."

209 Angalia kile Mungu alichomfanyia, Yeye alimbadilisha, akamfanya kijana tena, mke pia. Hakika, alifanya hivyo. Kweli kabisa. Ikiwa hiyo si kweli, waliposhuka kwenda Gerari, mbona, mfalme alimpenda maskini bi-kizee huyo? Akijitafutia mchumba, naye akasema, kitu kirembo zaidi alichopata kuona, kasema, "Unapendeza macho." Ati maskini bi-kizee? Hasha, aligeuzwa akawa mwanamke mchanga, ikionyesha kile hasa Mungu atamfanyia kila mmoja wa Uzao wa Ibrahimu. Haleluya! Kila mwanaume na mwanamke, haijalishi ilicho rika yako, na una umri gani, Mungu atakurudisha wakati fulani kuwa kijana mwanamume na mwanamke tena, kwa utukufu wa Mungu, maana wewe ni Uzao wa Ibrahimu. Loo, jamani. Jinsi ninavyopenda hilo.

210 Sasa, angalia, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma . . . " Sasa, tunamwona Ibrahimu akija mpaka Sodoma, Mungu alikuwa amemshughulikia kwa miaka yote kwa ishara na maajabu ya kila namna, lakini sasa ngoja, kama tu alivyofanyia Uzao wa Ibrahimu.

211 Tume—tumekuwa Pentekoste sasa kwa miaka hamsini, tumeona kunena kwa lugha, kufasiriwa kwa lugha, tumeona

uponyaji wa Kiungu, ishara, na kila kitu. Lakini sasa, ngoja kidogo, Sodoma inakaribia kuteketezwa, sio gharika ya Nuhu sasa, hii ni Sodoma, Yeye alisema.

212 Pia angalieni kuongezeka kwa utovu wa uadilifu ulimwenguni katika miaka michache iliyopita, miaka arobaini, ama yoyote ile. Angalieni jinsi unavyoongezeka kila siku, kila saa. Nikipitia Hollywood hivi majuzi, nilikuwa na, ama, wakati fulani uliopita, nilikuwa na ndege, nami nikasoma ambapo ushoga huko Los Angeles umeongezeka, au, huko California ulikuwa umeongezeka asilimia thelathini zaidi ya mwaka jana. Mnaona? Upotovu, kama tu Sodoma. Ulimwengu wote umegeuka kuwa hivyo, Pwani hii ya Magharibi, ambapo mashariki na magharibi zimekutana hapa. Mnaona? Hiyo ni kweli.

Kwa hiyo sasa tunaona tuko katika siku za mwisho, kama Ibrahimu, Uzao wake wa Kifalme umefika hadi siku za mwisho, kama vile Ibrahimu mwenyewe alivyokuja katika siku za mwisho.

213 Sasa, kumbukeni, daima kuna matabaka matatu ya watu, na hapa nitayataja, hao ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, wako katika kila umati. Kwa hiyo m—mnao. Kwa hiyo hao hapo, huyu hapa Ibrahimu, Kanisa lililoitwa litoke na kuteuliwa; Lutu, kanisa baridi, rasmi, huko chini Sodoma, pamoja na Wasodoma.

214 Ndipo siku moja, wakati saa ilipokaribia sana ya kuteketezwa kwa dunia wakati huo, Ibrahimu alikuwa ameketi chini ya mwaloni wake. Sasa, sikilizeni kwa makini sana, msilikose hili. Sasa, Yesu alisema itajirudia katika wakati wa mwisho, kabla tu Yeye hajaja.

215 Sasa, Malaika watatu walijitokeza, na Mmoja wao alikuwa ni Mungu. Kwa hiyo akaketi chini pamoja na Ibrahimu, kisha wawili wao wakashuka Sodoma na kuwahubiria Injili. Hiyo ni kweli? Billy Graham mamboleo kwa kanisa la kawaida lililoko Sodoma, watu mashuhuri kama hao, Oral Roberts, akishuka kwenda kule, akifanya. . .Hawakufanya miujiza mingi, sio mingi sana. Walifanya jambo fulani, kuwapofusha, kuhubiri Injili hupiga. . .Hao hapo katika milki hiyo ya kimadhehebu, wakashuka kwenda kule wakiihubiri Injili. Billy Graham yule mwinjilisti mashuhuri, hodari kwa Wabaptisti na Presbiteri, loo, yeye anawawekea mstari. Lakini mnaona, aliwahubiria, akiwaita watoke.

216 Lakini kulikuwa na Mmoja aliyebaki nyuma pamoja na Ibrahimu, Naye akampa Ibrahimu ishara. Sasa, sikilizeni kwa makini sana. Siku moja tu kabla ya hapo, jina lake lilikuwa Abramu, na jina la mkewe lilikuwa S-a-r-a-i, Sarai. Ndipo akabadilisha jina lake kutoka Abramu likawa Ibrahimu, baba wa mataifa; h-a-m, A-b-e-r-h-a-m, herufi saba, A-b-e-r-h-a-m,

Ibrahimu. Sasa, Yeye alibadilisha jina la Sara kutoka S-a-r-a-i likawa S-a-r-a, binti mfalme.

217 Sasa, hao Malaika wa—walioshuka kule, walishuka na kuhubiri Injili, na kuwaambia, "Tokeni—tokeni kwenye machafuko huko chini, tokeni miongoni mwake." Na je, si hivyo ndivyo Billy Graham, na hao watu mashuhuri, Jack Shuler, na hao jamaa siku hizi, wanavyoita kutoka Babeli kote ulimwenguni? Lakini yule Malaika aliyebaki na lile Kanisa ambalo halikuwahi kuwa Sodoma, angalieni aliyofanya kama ishara.

218 Sasa, Sara hakuwa kama wanawake wa kisasa wa siku hizi. Uh-uh. Aliketi kwenye hema. Kwa hiyo Malaika huyu akamwambia Ibrahimu, akasema, "Ibrahimu," sio Abramu, "Ibrahimu," Alijuaje jina lake lilikuwa Ibrahimu sasa? "yu wapi mkeo," S-a-r-a, "Ati Sara?" Alijuaje kuwa alikuwa ameoa? Vipi, Yeye alijuaje jina lake lilikuwa Ibrahimu, wakati lilikuwa ni Abramu? Alimjuaje Sara, mkewe (aliyekuwa Sarai), alikuwa Sara?

"Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?"

Ibrahimu akamtazama, akasema, "Mbona, yuko hemani nyuma Yako."

219 Akasema, "Ibrahimu, nitakurudia kulingana na wakati wa uhai. Mimi," kiwakilishi nafsi tena, Yeye yule, akampa jina. Mnaona? "Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai."

220 Naye Sara, ndani ya hema nyuma ya huyo Mtu, akasema, "Ati mimi, mwanamke mkongwe? Mbona," kasema, "sijapata raha na bwana wangu," mumewe hapo, "kwa, labda ilikuwa miaka ishirini." Kasema, "Mimi mwanamke mkongwe, na bwana wangu mzee pia? Ati tuwe na raha tena kama vijana?" Naye, kile tunachoita, akacheka kifichifichi, kwa namna fulani peke yake.

Naye huyo Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Whiu! Alimtisha vibaya sana. Ilikuwa ni nini?

221 Sasa, hiyo ilikuwa ni nini? Na Mtu huyo aliyezungumza na Ibrahimu, Ibrahimu alimwita Mungu, herufi kubwa B-w-a-n-a. Naye msomi yeyote wa Biblia anajua ya kwamba Huyo ni—ni Yeye Aishiye Peke Yake, Elohimu, mnaona, Mungu Aishiye Peke Yake.

Mtu fulani aliniambia, akasema, "Usingeamini huyo alikuwa ni Mungu?"

222 Nikasema, "Biblia ilisema alikuwa ni Mungu." Nikasema, "Mbona, hiyo ni nini kwa Mungu?" Nikasema, "Tumeumbwa kwa elementi kumi na sita, hizo ni kalisi, potashi, na petroli, na nurulimwengu."

223 Mungu alinyosha tu mkono na kuchota konzi la elementi za ulimwengu, kasema, "Whiu! Ingia humo ndani, Gabrieli, tunaenda chini huko Sodoma." Akanyosha na kuchota konzi

lingine, "Whiu! Ingia humo, Mikaeli," na, "Whiu!" akaingia Mwenyewe. Mbona, alifanya hivyo! Akala, akala—akamla ndama ambaye Ibrahimu alimchinja (Hiyo ni kweli?), akanywa maziwa, na kula ugali, na kula siagi. Hiyo ni kweli. Mungu! Vema, ni—nina furaha. Si kitu kwa Mungu, mnasahau tu Yeye ni Nani. Nina furaha sana.

224 Nimebakiwa na kama nywele nne ama tano tu, mnajua, na hivi majuzi nilikuwa nikizichana nywele hizo nne au tano, ndipo mke wangu akaniambia, akasema, "Billy, unaingia upara."

Nikasema, "Lakini sijapoteza hata moja ya hizo."

Akasema, "Ati nini?"

Nikasema, "Sijapoteza hata moja ya hizo."

Akasema, "Nakuomba, hebu uniambie ziliko."

225 Nikasema, "Sawa, mpenzi, nitakwambia. Wewe niambie zilikokuwa kabla sijazipata, ziko huko zikiningojea nizijie." Ndivyo ilivyo. Hiyo ni kweli.

226 Yeye alisema, "Kila unywele wa kichwa chako umehesabiwa. Hakuna kitakachopotea. Nitakifufua tena katika siku za mwisho." Yeye aliyenipa hizo sasa, hivi hawezi kunirudishia tena kwa ahadi? Kama anaweza kunifanya kile nilicho pasipo kujichagulia, ni zaidi sana vipi anaweza kunirejesha jinsi nilivyokuwa kwa chaguo, kwa kumchukua Yeye? Amina.

227 Loo, najisikia kubarikiwa sasa, naam, bwana, kujua ya kwamba ufufuo unakuja, nasi tutarejeshwa tena kama alivyomwonyesha Ibrahimu mle ndani. Angalieni. Sasa, Yesu alisema ya kwamba huyo alikuwa—huyo alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa mwanadamu.

228 Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Je, si ni ajabu hii, kwa kanisa hilo la kawaida huko nje, kamwe hatujawahi, katika nyakati zote, kamwe hatujawahi kuwa na mtu, mhudumu, katika makanisa hayo ambaye jina lake liliishia kwa h-a-m mpaka wa leo? H-a-m. Mnajua hilo, sivyo? Tumekuwa na Moody, Sankey, Billy Sunday, na Knox, Calvin, Spurgeon; Kote kote, tumekuwa na watu wa kila namna, lakini hakuna hata mmoja aliyeishia kwa h-a-m, G-r-a-h-a-m, kwa kanisa huko Sodoma. G-r-a-h-a-m, mjumbe kwa kanisa lililoko Sodoma, akionyesha kabisa Ujumbe uliokuwa . . . walifanya wakati huo. Basi hivi Yesu hakusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma . . . "? Huyo hapo Billy Graham, G-r-a-h-a-m, huko nje hudumani.

229 Sasa, Yeye anamtuma mjumbe kwa Kanisa lililoteuliwa, Wapentekoste walioteuliwa, waliovutwa watoke, si huko nje katika kanisa la kawaida, bali Kanisa lililoteuliwa. Nalo Kanisa Lenyewe ni Roho Mtakatifu akitenda kazi ndani ya Kanisa ndiye anayezitenda hizo kazi. Huo haukuwa mwili huo wa nyama, labda ulitoweka. Lakini ilikuwa ni Mungu katika mwili huo, akionyesha kwamba Mungu angeishi tena katika mwili

uliokombolewa wa Kanisa Lake katika siku za mwisho na kufanya ishara iyo hiyo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Haleluya! Haya basi, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

230 Loo, hakika. Ungeona nini? Dhihirisho la Neno. "Nalo Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo." Enyi marafiki, huyo alikuwa ni Yesu jana. Na kama Neno likidhihirishwa tena leo, si litakuwa ni Yesu leo? Je, ingekuwa vivyo hivyo jana. . .? Ni wangapi wanaoamini hivyo? Hebu tuombe.

231 Baba wa Mbinguni, Uwepo Wako mkuu, adhimu uko hapa ndani ukiwafurahisha watoto Wako, ukiyamimina mafuta ya imani moyoni mwao, kupokea baraka za Mungu zilizowekwa kwa ajili yao. Sasa, tunaitwa kwa Jina Lako, nawe ulisema kama tungekusanyika na kuomba, kwamba ungesikia kutoka Mbinguni, uiponye nchi. Nasi hapa, usiku wa leo, hapa juu kabisa, mwishoni mwa barabara, huku nje visiwani, huku nje kabisa kupita Pwani ya Magharibi, huku nyuma kabisa. Nawe ulisema . . . nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni."

232 Wakiketi katika jengo hili, usiku wa leo, ni Wahindi ambao Wewe uliwaweka hapa, na siri yake unayo Wewe, jinsi ulivyowaweka hapa, bali Wewe uliwaleta hapa. Tuko moja kwa moja kwenye mpaka wa maji. Nasi tunamwona mjumbe ambaye amekwenda kwa Uzao ulioitwa wa Ibrahimu, kanisa likiwa mahali pake, ambalo limetoka huko nje Babeli, akionyesha ishara yake huko nje.

233 Ee, Bwana, tunaomba, usiku wa leo, kwamba katika Jina la Yesu kwamba utalifanya kundi hili dogo la watu lijue kwamba Wewe hujafa, umefufuka katika wafu, na miaka elfu mbili ya ukosoaji isingeweza kukuondoa Wewe. Ungali hapa, ukithibitisha kwamba Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele.

234 Baba wa Mbinguni, kundi la kupendeza la watu hapa, wameketi katika jengo hili lenye joto, na sasa, wape thawabu, Bwana nami ninatazama kwa matarajio ya kitoto, kwa moyo kama wa mtoto wakati wa Krismasi, nikingoja. Kamwe. . . Miaka hii yote, Bwana, hujatupungukia kamwe, lakini hata hivyo, moyo wangu unaruka kila ninapowazia juu ya Wewe kuja Mbele Zetu, ama sisi Mbele Zako. Sasa, ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utaingia mioyoni mwetu.

235 Wape watu hawa imani, usiku wa leo, kuamini. Na ujalie sasa kwamba utanipa imani, Bwana. Lakini imani yangu bila yao isingefaa kitu, hatuna budi kuwa na imani pamoja, kwa sababu sisi ni kitu kimoja, sisi ni Mwili wa Bwana Yesu. Na tumekusanyika pamoja katika ukumbi mdogo uliokodishwa

usiku wa leo kama walivyofanya katika siku zilizopita, miaka elfu mbili iliyopita.

236 Na sasa, tuliomba katika chumba hiki cha juu, usiku wa leo, ya kwamba utaingia humu ndani na kuwaonyesha, watu hawa, ya kwamba Wewe ungali hai. Basi, Baba, kama utafanya tu hivyo, kila mtu hapa ndani ataondoka akiwa na furaha, wataondoka wakiamini kwa ajili ya magonjwa yao na kusamehewa dhambi zao, watakuwa na ujasiri. Hawa. . . Wengi wa watu hawa maskini ambao hata hawana chakula cha kutosha, labda, na baadhi yao wana—wanaishi maisha duni kabisa, wengine labda, Bwana, wanahangaika tu siku baada ya siku. Nasi sote ni maskini, Bwana, nasi tuna—tunajaribu—tunajaribu kuifanya Mbingu Makazi yetu.

237 Njoo kati yetu usiku wa leo, Baba. Maneno haya ambayo nimehubiri, yataanguka tu kando ya njia ikiwa Wewe hutakuja na kuyathibitisha. Tujalie, Bwana. Tutakushukuru Wewe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

238 Sasa, nitawaambia. . .Ni saa nne kasorobo. Je, mwaweza kunipa mstari mdogo, mfupi tu wa maombi, kama dakika kumi na tano? Hebu. . .Je, mtafanya hivyo? Sawa. Sasa, naamini Billy alisema alisambaza, ngapi? Takriban kadi hamsini za maombi? Vema.

239 Sasa, kadi za maombi. . .Kila mtu, aliye na kadi ya maombi, ishikilie namna *hii*. Ni kadi ndogo tu ya maombi yenye nambari juu yake, ina namba kwenye hiyo kadi ya maombi. Na sasa, tungependa kuona. . .Hebu tuone, tuanzie wapi? Tuanzie moja, usiku wa leo. Moja mbili, tatu, nne, tano. Hebu tuwaone wakisimama. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye na namba moja, mbili, tatu, nne, tano? Hebu tuone mkono wako. Moja, mbili, tatu. Hebu tuone mwingine. Moja, mbili, tatu, nne, tano.

240 Una hakika watu wote wanajua Kiingereza? Wote wanajua Kiingereza? Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Inua mkono wako. Namba moja, namba mbili, mbili. Mhindi angesemaje mbili, kama angelisema kwa lugha yake mwenyewe? Sawa. Mlisikia. Namba mbili, kadi ya maombi namba mbili? Namba tatu, nani aliye na namba tatu? Mama huyo anayo nambari tatu. Namba nne, ni nani aliye na namba nne, kadi ya maombi? Yule mama pale. Sawa.

241 Hakika kuna moja, mbili, au tatu hapa mahali fulani. Angalieni, kila mtu aangalie kadi za mwenzake. Angalieni vizuri. . .Kila mtu, aliye na kadi, inua mkono wako. Kila mtu, aliye na kadi ya maombi, inua mkono wako. Sasa, angalieni kila mmoja kadi ya mwenziwe. Angalia. . .Mnaona, labda hawawezi kusikia. Mnaona inawezekana awe ni mtu fulani kiziwi, na—nami niwapite. Mnaona? Wao. . .Au labda hawawezi kutembea, wamelemaa na hawawezi kutembea. Moja, mbili. Ni nani aliye

na moja au mbili? Tatu, yule mama anayo. Nne, tunayo. Sawa. Tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Sawa. Hebu wasimame waje huku. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, hebu waje tu papa hapa kwenye kona. Hilo ni jema. Moja mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba.

242 Kuna kadi tatu ambazo hazipo sasa. Kuna tatu hazipo sasa. Mnaona, sababu ya mimi kutaka kupata kila mmoja wao, kwa sababu mtu anaandika na kuniambia baadaye, kasema, "Vema, hakuna mtu aliyeniambia. Nilikuwa kiziwi. Nisingeweza kuamka wala hakuna mtu aliyeniambia." Mnaona? Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi.

243 Huyu hapa mwingine, jamaa huyu hapa. Sasa, namba yake ni ipi? Mbili? Sawa, moja. Moja, kadi ya maombi moja? Tulipata mbili, tatu. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Tumekosa moja. Namba moja? Vema, endapo walitoka, labda walitoka nje, nao watarudi ndani, baada ya dakika moja tu. Vema. Wakifanya hivyo, wanayo nafasi yao kwenye mstari.

244 Sasa, kumbukeni, kila mtu anayeshika kadi ya maombi, kama hatutaifikia usiku wa leo, tutaifikia, nasi tutamwombea kila mtu anayekuja kwenye mkutano na anataka kuombewa.

245 Sasa, hebu tuone. Hao ni kumi, tisa. Hebu tuone kumi, kumi na moja. Ni nani aliye na kadi ya maombi kumi na moja? Hapana? Kumi na mbili? Sawa, bwana. Kumi na tatu, kumi na nne? Vema, mama, hapa. Kumi na tano?

246 Sasa, unapokuja . . . Hebu niseme hivi. Mnaona? Sasa, unapokuja na kupata kadi, ishikilie. Unaona? Usiibadilishe, kumpa mtu; inakupasa uwe hapa ujitwalie mwenyewe. Chukua kadi yako na uishike. Unaona? Unaona, mtu mwingine angeweza kupachukua mahali hapo. Unaona? Ukipata kadi, ishikilie. Hatujui tulipo . . . Roho Mtakatifu atatufanya tuvute, na sisi—sisi tunakutaka huko kwenye wakati huo. Kwa hivyo wewe njoo, uchukue kadi yako.

247 Hebu tuanze moja kwa moja na hao. Wengine wanaingia, na tuna kama wawili ama watatu ambao hawapo, lakini hiyo itakuwa ni sawa. Sasa, tunataka u—uamini sasa kwa moyo wako wote.

248 Sasa, nataka usikivu wenu hapa. Ni wangapi humu jengoni ambao ni wagonjwa, wala hawana kadi ya maombi na hawataitwa mstarini? Inueni mikono yenu. Hebu tuone. Kila mtu? Kweli, ni karibu tu kote huku.

249 Sasa, hapa, sasa wakati wanapoupanga mstari huo wa maombi kupitia kwenye chumba hicho hapo, ninataka kuwaombeni jambo fulani. Sikilizeni sasa, kwa makini sasa. Sasa, yote niliyosema yataenda bure ikiwa sivyo. Kama . . . Mtu yeyote anaweza kusema chochote. Lakini kama Mungu . . . Kama haliko kwenye Neno la Mungu, kwanza kabisa usiliamini, lakini

kama ni Neno la Mungu, basi mtazamie Mungu kutimiza ahadi hiyo, maana Mungu hana budi kutimiza ahadi Yake kusudi awe Mungu. Ikiwa nitakuwa mwaminifu, sina budi kutimiza ahadi yangu. Mnaona? Mtu wa heshima—mtu wa heshima sikuzote hutimiza neno lake. Mnaona? Wewe sikuzote hutimiza neno lako.

250 Sasa, kila mmoja wenu huko nje, ambaye hayuko katika mstari huu wa maombi, wala hatakuwa ndani yake, msio na kadi za maombi, angalieni tu huku. Hebu nikwambie la kufanya.

251 Kulikuwa na maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, katika Biblia. Nitawapa hadithi ndogo. Yeye pia hakuwa na kadi ya maombi, bali alimwona Yesu akivuka bahari, na alikuwa kule chini, mtu mmoja akamwambia Yeye alikuwa huko chini. Naye aliamini kama angegusa tu vazi Lake kwamba angeponywa. Je, umewahi kuisikia hiyo hadithi? Ni wangapi wamewahi kuisikia? Hakika.

252 Huyo mwanamke aligusa. . . Alikuwa anatokwa na damu. Na sasa, kumbukeni, nami nimekuwa katika nchi hiyo, vazi la Wapalestina linapwaya, ni joho, nalo lina vazi la ndani, kuzuia vumbi maungoni.

253 Sasa, kama aligusa upindo wa vazi Lake, kimwili, Yeye hakuuhisi huo, mnajua ninachomaanisha, Hakuuhisi katika mwili Wake. Lakini alisema moyoni mwake, "Naamini Yeye ni Mtu mtakatifu, na endapo ninaweza tu kumgusa, nitapona." Je, hiyo ni kweli? Naye alikuwa anatokwa na damu.

254 Ndipo akajipenyeza kwenye umati, naye akainama, akaugusa upindo. Huo ulikuwa mbali *hivi* na miguu Yake, ambapo vazi hilo hupembelea nje. Naye akagusa upindo wa vazi Lake, kisha akainuka, akarudi nyuma, na labda akaketi kwenye kusanyiko, ndipo Yesu akasimama, akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?"

Nanyi mnajua Petro alisema nini? Petro akamkemea, akasema, "Bwana, kwa nini unasema jambo kama hilo?" Kasema, "Vema, kila mtu anakugusa Wewe."

"Aloo, Rabi, Nabii mkuu wa Mungu." "Ewe mdanganyifu." Kila mtu, mnaona, kila mtu anamgusa.

Akasema, "Kila mtu anakugusa Wewe. Kwa nini useme 'Ni nani aliyenigusa?'"

255 Akasema, "Lakini naona nimekuwa dhaifu. Nguvu," uweza, "ulinitoka, nimekuwa dhaifu." Maskini mwanamke huyo mmoja alimgusa na kumfanya dhaifu. Naye akageuka, kisha akaangalia juu ya wasikilizaji mpaka akampata, akamwambia shida yake ilikuwa nini, na kusema imani yake ilikuwa imemponya. Je, hiyo ni kweli?

Sasa, huyo alikuwa ni Yesu Kristo jana. Je, hiyo ni kweli? Vema, kama Yeye ni yule yule leo, Yeye si atafanya vivyo hivyo?

256 Sasa, kwa ajili ya ndugu zangu wahudumu, wanaweza kutaka Andiko kwa hilo, nitawapa moja sasa. Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 3, kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, leo hii, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli, ndugu? Ni wangapi wanaojua hiyo ni Kweli, Biblia inasema hivyo? Kwamba Yeye ni nanii Mkuu. . . Vema basi, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetendaje leo? Kama alivyotenda wakati huo. Je, hiyo inamfanya Yeye yule jana, na hata milele?

257 Basi sasa, kama ukija hapa na kunigusa, mimi ni kama baba yako, ama ndugu yako, mume, ama yeyote yule, haingefaa kitu hata kidogo, mimi ni mwanadamu tu, mguse mchungaji wako, jambo lile lile. Bali wewe mguse Yeye uone Roho akishuka chini. Mnaona? Amina. Jambo ndilo hilo, mnaona. Hilo linamfanya Yeye yule jana, na hata milele. Isingekuwa mimi, ingekuwa ni karama anayotumia kutenda kazi.

258 Ndugu Wood, je, ulikuja na picha hizo au chochote? U—unazo? Loo, ulikuwa nazo pale jukwaani? Mliziona usiku wa leo? Tutakuwa nazo kesho usiku. Mngetaka kuiona picha Yake namna gani? Tunayo papa hapa, ndugu. Hivi sasa, imening'inia Washington, DC, iliyo na hatimiliki, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha, Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, Hii hapa. Nayo itafanya kazi ile ile iliyofanya.

259 Yesu alisema, "Nilitoka kwa Mungu na nikaenda kwa Mungu." Alikufa, akafufuka, akapaa Mbinguni. Naye Paulo, akienda zake Dameski, Nguzo kubwa ya Moto ilimpofusha. Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Je, hiyo ni kweli? Yeye yule jana, leo, na hata milele.

260 Sasa, wewe usiye na kadi ya maombi, wewe angalia huku, nawe uanze tu kuomba. Anza kuomba, ukisema, "Bwana Yesu, ninakuamini. Na maskini mzee huyo aliyesimama hapo, jukwaani, hanijui."

261 Vema, hakuna mtu katika jengo hili ninayemjua, nje ya Ndugu Wood, ninamwona amesimama huko nyuma. Ninaamini hao ni, ndugu kadhaa hapo, Ndugu Fred Sothmann kutoka Canada hapa, ninamfahamu. Lakini hakuna mtu katika eneo hili hapa, hapo. . . Ni wangapi kati yenu hapo ambao hatufahamiani? Inueni mikono yenu. Kila mtu aliye mgeni, nawe unajua kwamba sikujui, inua mkono wako. Ninyi watu katika mstari wa maombi, mnaojua hatufahamiani, inua mkono wako. Mnaona? Sawa.

262 Sasa, wewe amini tu na kusema, "Bwana Yesu, kwa imani ninaamini ya kwamba aliyosema ndugu huyo ni Kweli. Mimi ni mgonjwa, Bwana, jalia nikuguse Wewe." Na kisha useme. . . Kutenda juu Yake. Mwangalieni Roho Mtakatifu akishuka moja

kwa moja kupitia hapa na kufanya jambo lile lile alilofanya. Kama halifanyi, basi mimi ni nabii wa uongo. Kama akifanya hivyo, basi wewe liamini. Hiyo ni kweli.

263 Sasa, mtu huyu hapa, ulimpa huyo mvulana kadi yako hapo ndani? Naam, sawa. Unazungumza Kiingereza vizuri? Ha—hatufahamiani. Ninaamini yeye ni ndugu wa Kihindi. Je, huyo...Mhindi? Vema, sisi hapa, wageni wawili, wanaume wawili, hatujawahi kukutana hapo awali maishani. Sasa, yeye anasimama hapa, yeye ni mwanadamu tu, ninasimama hapa kama mwanadamu. Yuko hapa kwa sababu nisizofahamu. Sijawahi kumwona, nami...vema, hii ndiyo mara yetu ya kwanza.

264 Lakini sasa, kama Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, anaweza kuwa...naye mtu huyu anaweza kuwa hapa kwa ajili ya, labda ni mahitaji ya kifedha, labda ni shida ya kinyumbani, kitu kibaya nyumbani kwake. Huenda ikawa yeye ni mgonjwa, au labda amesimama hapa kwa niaba ya mtu mwingine. Sijui, sijawahi kumwona. Lakini sasa, kama alikuwa amesimama hapa, nami nikasema, "Utukufu kwa Mungu. Haleluya! Mungu alinituma kuwaombea wagonjwa," nimwekee mikono. Ningesema, "Wewe ni mgonjwa, bwana?"

Angesema, "Naam, mimi ni mgonjwa."

265 Nimwekee mikono, niseme, "Utukufu kwa Mungu. Nenda, ukapone." Hiyo ingekuwa sawa. Lakini vipi kama Roho Mtakatifu akishuka hapa, na kumwambia kile ambacho amekuwa? Atajua kama hiyo ni kweli au la. Na kama Yeye anajua kile ambacho amekuwa, hakika anaweza kuamini atakachokuwa, kama Yeye anaweza kumwambia yale ambayo yamekuwapo. Je, hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wangeamini jambo hilo kwa moyo wako wote? Useme, "Nitakubali." Sasa, Bwana Mungu na alijalie.

266 Ninataka tu uangalie huku, bwana, kuzungumza tu nawe kwa dakika moja, huku hatufahamiani. Na kama kuna njia yoyote ambayo ningeweza kukusaidia, ningekusaidia. Lakini ikiwa Bwana Mungu anaweza kuniambia, kama, kile kilichokuleta hapa, yale umefanya, kilicho katika... ulichopaswa kufanya, ama shida uliyo nayo, ama chochote kile, ungejua kama hiyo ilikuwa ni kweli au la. Na kwa hiyo, basi sisi...Ingelifanya hili kusanyiko kuamini. Ikufanye wewe kuamini, sivyo? Maana unajua ningekuwa...Nisingeweza kulifanya mimi mwenyewe, maana mimi ni mwanadamu tu, kama ulivyo wewe, ingebidi iwe ni nguvu fulani za kimbinguni. Na ikiwa ni nguvu za kimbinguni...

267 Sasa, Mafarisayo wa siku hizo walisema i—ilikuwa ni Beelzebuli, ibilisi, angalieni kilichowapata. Hao walioamini ilikuwa ni Kristo, walipokea thawabu ya Kristo.

268 Sasa, ninawaambia sasa, mtu huyu, aliyesimama hapa, anapitia magumu. Hiyo ni kweli. Amesimama hapa kwa sababu ni vigumu kujua aelekee wapi, kwa sababu ni jambo la kigeni, ni mara ya kwanza katika nchi hii. Usifadhaike, bwana, Huyo hatakudhuru, Huyo ni Kristo. Hebu nikuonyeshe ya kwamba Ndiye. Unaona? Uko hapa kwa ajili ya uponyaji, wewe ni dhaifu, umekuwa na shida fulani, umekuwa kwenye chumba cha upasuaji. Ulifanyiwa upasuaji, na huo ulikuwa ni wa vidonda kwenye tumbo, nawe umedhoofika sana kwake. Nawe uko hapa kwa ajili ya…Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Yote yamekwisha, nawe utapona. Mungu akubariki. Imani yako inakuponya.

269 Unaamini? "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. Tunataka kumwona Yesu." Sasa, pengine marafiki zake Wahindi huko nje walimjua. Kama—kama unaweza kuamini tu. Vema.

270 Sasa, huyu hapa mwanamke kutoka kwa Waanglo-Sakson. Sasa, huyu hapa mwanamume na mwanamke, nadhani hatufahamiani, tumeninii…mara ya kwanza tumekutana. Sasa, simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye ni mgeni. Na sasa, labda tuna…Yeye ana umri mkubwa kidogo kuliko mimi, na sisi ni—sisi ni…tulizaliwa umbali wa maili nyingi na tumeachana kwa miaka mingi, na hii ndiyo mara ya kwanza tunakutana. Lakini sasa, kama Roho Mtakatifu wa Mungu atanijulisha sababu ya wewe kuwa hapa, ama jambo fulani kukuhusu, ambalo unajua kwamba sijui, basi, itakufanya uamini, sivyo? Vema. Amini tu sasa.

271 Huyu mama, ninamwona ameketi mezani, la, anarudi nyuma. Ni tumbo lake, ana tatizo la tumbo. Hiyo ni kweli kabisa. Kidonda cha tumbo, nacho husababisha mchomo, asidi, na kadhalika. Una fadhaa, inakufanya usononeke, jioni sana unachoka sana na kuvurugikiwa. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Je, hilo lingekusaidia? Binti Berling. Na…Hiyo ni kweli. Vema. Nenda zako, amini sasa, hilo tatizo la tumbo litakuacha nawe utapata afya.

272 Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Vema…?…Amini tu. Usitie shaka. Vema. Sasa, sasa, hiyo inanifanya kudhoo-…

Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu SWA62-0724
(Sir, We Would See Jesus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne jioni, tarehe 24 Julai, 1962, kwenye Jumba la Mikutano la Legion huko Port Alberni, British Columbia, Canada, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org